Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo



## Naibu Rais akanusha tuhuma za ufisadi Kenya

Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00084 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Oktoba 9-15, 2024 |

# Balozi wa Italia nchini ammwagia sifa Samia

- Asema anasimamia vizuri uchumi, maendeleo ya nchi

Uk. 4







Rais Samia Suluhu Hassan, (Picha kubwa kushoto) akizungumza na viongozi mbalimbali kabla ya kuzindua Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, (Chini kulia) akiwa pamoja na viongozi pamoja na wajumbe wa Tume hiyo, Ikulu jijini Dar es Salaam, wiki iliyopita. Picha ya juu kulia, Dk. Mwigulu Nchemba akiwa na Balozi wa Italia nchini.

## Dk. Samia atoa ruzuku mitungi ya gesi ya REA

Uk. 4



## Ziara ya Dk. Nchimbi Itimila 'yafunga' ofisi za Chadema





## Msekwa: Mkongwe aliyeshuhudia mengi kwa Nyerere

Uk. 12

## Makubwa yamefanyika miaka 25 bila uwepo wake

Uk. 10

## Tumuenzi kwa kuchagua viongozi bora

Uk. 11

## Alianza JPM, Samia anakamilisha Dodoma aliyoitaka Mwalimu



Uk. 14

rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com

# Dk. Mpango aahidi neema za kijamii Igunga

**Na Mwandishi Wetu, Tabora**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, amesema serikali itaendelea kuboresha huduma za kijamii zikiwemo za maji, elimu, afya na miundombinu ili kurahisisha shuguli za kiuchumi katika Wilaya ya Igunga mkoani Tabora.

Dk. Mpango alitoa ahadi hiyo mbele ya wananchi wa wilaya hiyo waliojitokeza kumpokea eneo la barabara ya Mwanzugi akianza ziara ya kikazi ya siku nne mkoani Tabora jana.

Aidha, Makamu wa Rais aliwapongeza wananchi wa wilaya hiyo kwa kufanya kazi kwa bidii na kuwa wazalishaji wazuri wa mazao ya chakula, biashara na ufugaji.

Kadhalika, aliiagiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kushughulikia ujenzi wa soko la kisasa na Kituo cha Mabasi cha Wilaya ya Igunga.

Kuhusu upungufu wa watumishi katika sekta mbalimbali wilayani humo, aliiagiza Tamisemi kutoa kipaumbele kwa wilaya hiyo wakati wa upangaji wa watumishi.

Na katika hatua nyingine, Dk. Mpango aliwataka wananchi wa maeneo hayo kuhakikisha wanatilia umuhimu elimu kwa watoto badala ya kuwaacha washiriki shughuli za uchimbaji madini.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Igunga (hawapo pichani), katika siku yake ya kwanza kati ya nne ya ziara ya kikazi mkoani Tabora jana.

> "Dk. Mpango alitoa ahadi hiyo mbele ya wananchi wa wilaya hiyo waliojitokeza kumpokea eneo la barabara ya Mwanzugi akianza ziara ya kikazi ya siku nne mkoani Tabora jana.

# Bashe azindua kiuatilifu hai rafiki wa mazingira



**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo Hussein Bashe, amezindua kiatilifu hai cha Thurisave-24 ambacho ni rafiki kwa mazingira kinachoangamiza wadudu waharibifu wa mazao mashambani.

Kiuatilifu hicho kinatengenezwa na Kiwanda cha Viuatilifu hai cha Tanzania Biotech Products Ltd (TBPL) kinachomilikiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kilichopo Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani.

Waziri Bashe alisisitiza umuhimu wa kutumia viuatilifu hivyo na kumuelekeza Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya viuatilifu, zinatumika kununua bidhaa za TBPL na kuwafundisha wakulima jinsi ya kuvitumia ipasavyo.

Thurisave -24 inatumika kwenye mazao ya mahindi, pamba, tumbaku, viazi vitamu, viazi mviringo, mihogo, kabeji, mbogamboga za majani, matunda na maharage.

Kwa mujibu wa tafiti zilizofanyika, kiuatilifu hicho kisicho na madhara, huangamiza wadudu waharibifu wa mazao katika hatua ya viwavijeshi na huleta ufanisi wa hali ya juu katika udhibiti wa viwavi wa jamii ya Lepidoptera.

Waziri Bashe alisema Thurisave inahakikisha usalama wa ikolojia na afya za watumiaji kwa kuwa haina sumu dhurifu na ni rafiki wa mazingira hivyo kutimiza Malengo ya Milenia.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa pia na Balozi wa Cuba nchini, Yordenis Vera.

# Ziara ya Dk. Nchimbi Itimila `yafunga' ofisi za Chadema

**Na Mwandishi Wetu, Itimila**

MWENYEKITI wa Chadema Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, Terry Kilugala na Katibu wake, Gershom Migasa Mipawa pamoja na wanachama zaidi ya 60, wamehamia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Viongozi na wanachama hao, walipokelewa na Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, katika mkutano wa hadhara uliofanyika eneo la Luguru wilayani Itilima.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Kilugala alisema mbali na Chadema kuwatumia vibaya viongozi na wanachama wake na kuwaacha 'watupu' wakiangaliana wenyewe kwa wenyewe, uongozi wa CCM na utendaji kazi wa Serikali inayoongozwa na Mwenyekiti wake Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ndivyo vilivyomvutia `arejee' nyumbani.

"Tulikuwa tunakwenda Mwanza siku mbili kwa ubovu wa barabara, leo tunaenda na kurudi. Lazima tuseme ukweli, CCM imefanya kazi, lakini wenzetu wamebaki kusema uongo na kututumia vibaya. Kuna wabunge wa Covid-19, lakini ndani yake wamo wake zao, halafu huku wanatudanganya," alisema.

Akiwapokea viongozi na wanachama hao kutoka Chadema, Balozi Nchimbialisema:

"Hawa ndugu zetu wameona mbali mapema, maana viongozi wakubwa kama Peter Msigwa kaona shida zao, wewe unasubiri nini? Rudini CCM na nawapongeza wote mliojiunga na CCM, viongozi pamoja na wanachama. Karibuni sana tufanye kazi ya kujenga taifa pamoja."



# Serikali yatenga bil. 18.5/- ujenzi Chuo Kikuu Songea

**Na Mwandishi Wetu, Songea**

SERIKALI inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imetenga Sh. bilioni 18.5 kujenga Chuo Kikuu cha Uhasibu mkoani Ruvuma.

Meneja wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Songea, Dk. Bakari Mashaka, alisema hayo juzi wakati wa hafla ya kugawa mipira saba kwa timu za mpira wa miguu za Mtaa wa Pambazuko, Kata ya Tanga, Manispaa ya Songea.

"Tunaleta mradi mkubwa wa takribani Sh. bilioni 18.5, ni fedha za Serikali kupitia Rais Dk. Samia ambaye ameweka lengo kila mkoa uwe na chuo kikuu," alisema.



**Mipira ya Miguu saba iliyotolewa na Chuo cha Uhasibu Arusha kwa timu za mpira wa Miguu zilizopo katika mtaa wa Pambazuko Kata ya Tanga, Manispaa ya Songea.**

Alisema chuo hicho kitakapokamilika, kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi kuanzia 5,000 mpaka 10,000.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa mapema kuanzia sasa mara baada ya taratibu za zabuni kukamilika na umepangwa umalizike baada ya miezi 18.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Pambazuko Nickson Mhagama, alisema wananchi wa kijiji hicho wameupokea mradi huo kwa furaha kubwa na wataendelea kushirikiana na chuo katika utekelezaji wa mradi huo.

Aliushukuru uongozi wa Chuo Kikuu hicho kwa kuwaelimisha wananchi juu ya faida za mradi huo.

Chuo cha Uhasibu Arusha kina eneo lenye ukubwa wa takribani hekta 26.5 katika Mtaa wa Pambazuko, Kata ya Tanga Manispaa ya Songea.

# Kampuni kuwekeza tril. 3.2/- miradi ya kusafirisha umeme

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI imeanza mazungumzo na kampuni mbili za kigeni zenye nia ya kuwekeza jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.2 (sawa na Sh. trilioni 3.2) kwenye miradi ya kusafirisha umeme, kupitia Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Kampuni hizo tayari zimeshaanza mazungumzo na Kituo cha PPP kuhusu uwekezaji huo.

Iwapo watafanikiwa, hii itakuwa ni mara ya kwanza kwenye historia ya nchi kutokea uwekezaji mkubwa wa njia za kusafirisha umeme kupitia ubia PPP.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha PPP, David Kafulila, alisema kuwa Serikali kwa sasa inajifunza kutoka kwa nchi za Latin America na Asia zenye uzoefu mkubwa wa ushirikiano wa sekta za umma na binafsi kwenye ujenzi wa miundombinu ya umeme.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni India, Peru, Chile, Brazil na Philippines.

"Majukumu ya Kituo cha PPP ni pamoja na kuratibu na kuchambua miradi yote ya uwekezaji wa ubia kati sekta ya umma na sekta binafsi," alisema.

Alisema Tanzania inakabiliana na changamoto kadhaa kwenye eneo la ubia PPP katika miradi ya kusafirisha umeme, ikiwemo masuala ya kanuni, sheria na upungufu wa uzoefu na utaalamu husika kwenye baadhi ya taasisi za umma.

"Kuna haja ya taasisi za umma na watumishi wa umma, kujengewa uwezo ili serikali ishiriki kikamilifu kwenye ubia PPP ndani ya sekta ya nishati," alisema.

Alisema baadhi ya wadau wa maendeleo, wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa miradi ya ubia PPP kwenye ujenzi wa njia za kusafirisha umeme katika nchi za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania, Uganda na Kenya.

"Uzoefu wa wachumi wa nishati unaonesha kuwa sekta ya nishati inaweza kujitegemea kujiendesha yenyewe kifedha iwapo bei ya umeme itapangwa kibiashara.

"Tanzania inauza umeme kwa bei ndogo kuliko nchi zote za Afrika Mashariki, ndiyo maana inaongoza kuwa na uchumi jumuishi kwenye eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Wizara ya Nishati ilitangaza mwaka 2022 kuwa Serikali inahitaji Dola za Marekani bilioni 1.9 (zaidi ya Sh. trilioni tano) kuimarisha njia za kusafirisha umeme nchini.

Alisema Tanzania kwa sasa inazalisha umeme wa ziada, lakini inashindwa kuusafirisha umeme wa ziada kwenda kwenye maeneo ya ndani na nje ya nchi yenye uhaba wa Nishati hiyo kutokana na upungufu wa njia za kusafirisha.

Alisema ubia wa PPP kwenye ujenzi wa njia za kusafirisha umeme, utaleta manufaa makubwa kwenye uchumi wa taifa.




**Baadhi ya wananchi wa Jimbo la Paje Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja, wakiwa katika moja ya vituo kujiandikisha na kuboresha taarifa zao kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura juzi. Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Zanzibar, ulianza juzi na utahitimika Oktoba 13, mwaka huu. Vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni. (Picha na INEC).**

# Hungary yampa `tano' Dk. Tulia amani duniani



**Na Mwandishi Maalum**

RAIS wa Hungary, Tamas Sulyok, amesema Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, anafanya kazi kubwa ya kutafuta amani katika nchi zilizokumbwa na migogoro duniani.

Alisema hayo alipozungumza na Dk. Tulia ambaye pia ni Spika wa Bunge la Tanzania jijini Budapest, juzi.

Katika mazungumzo yao, viongozi hao walijadili njia bora za kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na Hungary kwenye sekta mbalimbali.

Pia walizungumzia masuala yanayohusu misingi na malengo ya IPU, ambapo Rais Sulyok aliahidi kuendelea kushirikiana kwa karibu na kuwa mstari wa mbele katika kuendeleza ajenda zote za IPU.

# Balozi wa Italia nchini ammwagia sifa Samia

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa Italia nchini, Giussepe Sean Coppola, amempongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia vizuri uchumi na maendeleo ya nchi ikiwemo kuunda Tume ya Kushughulikia Changamoto za Kikodi nchini.

Alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba na ujumbe wake katika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha jijini Dar es Salaam jana.

Pongezi hizo zimekuja siku tano tangu Rais Dk. Samia alipozindua Tume ya Rais ya Kutathmini na Kushauri kuhusu Masuala ya Kodi iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam, Oktoba 4, mwaka huu.

Balozi Coppola alisema anaamini matokeo ya tume hiyo yataongeza chachu ya kufanya biashara na uwekezaji hapa nchini, hatua itakayochochea ajira, ukuaji wa uchumi na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kuchochea maendeleo ya nchi.

Aliahidi kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa kuchangia utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo kwa kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la kahawa nchini.

Italia imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo kwa Tanzania kutokana na kufadhili miradi mbalimbali kupitia Bajeti Kuu ya Serikali, ikiwemo miradi ya maji, afya, mafunzo ya ufundi stadi na huduma katika sekta za utalii na hoteli, uchumi wa buluu na usawa wa kijinsia.

Kwa upande wake, Waziri Dk. Nchemba alitoa wito kwa wawekezaji kutoka Italia kutumia mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo hapa nchini kuwekeza mitaji yao katika miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ili kukuza uchumi wa pande hizo mbili.

Alisema Serikali imeweka vivutio mbalimbali vya uwekezaji na kuialika sekta binafsi ya Italia, kushirikiana na Serikali kwa kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa miradi mbalimbali hapa nchini ukiwemo mradi wa Reli ya kisasa (SGR).



**Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba akisalimiana na Balozi wa Italia nchini, Giussepe Sean Coppola, jijini Dar es Salaam jana.**

# Rais Samia atoa ruzuku mitungi ya gesi ya REA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa ruzuku ya bei kwenye mitungi ya gesi inayotolewa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) ili Watanzania watumie nishati safi na salama kwa afya zao pamoja na kuhifadhi mazingira nchini.

Mkurugenzi wa Teknolojia Mbadala na Nishati Jadidifu, Mhandisi Advera Mwijage alisema hayo wakati akimwelezea Mkuu wa Wilaya ya Gairo na wananchi baada ya kutembelea banda la REA kwenye Maonesho ya Samia Kilimo Biashara Expo 2024 yanayofanyika Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro.

"Rais Samia ametoa ruzuku ya bei kwenye mitungi ya gesi ili iuzwe kwa bei rafiki, kusambazwa kwa wingi na kila Mtanzania aimudu na atumie nishati hii muhimu," alisema.




Aidha, REA itaendelea kusambaza kwa wingi majiko ya gesi nchini na Wilaya ya Gairo pekee jumla ya majiko 3,225 ya gesi yatatolewa kwa wananchi ikiwa ni sehemu ya kuitangaza na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema REA wameanza kutoa majiko banifu 790 kwa wananchi wa Gairo ambayo ni majiko rafiki, imara kwa muda mrefu, yanatunza mazingira na yanatumia kiasi kidogo cha mkaa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa ruzuku ya bei kwenye mitungi hiyo kwa wananchi wake ambapo itarahisisha upatikanaji wake kwa wingi.

"Wananchi wenzangu wa Gairo, majiko haya ni rafiki kwa matumizi, salama kwa afya zenu, ni msaada mkubwa katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira yetu. "Nawahimiza kuyanunua ili nishati hii iwe na manufaa makubwa kwenye familia zetu badala ya kuendelea kukata miti kupata mkaa na kuni," alisema.

# Serikali kuhakikisha nishati safi ya kupikia inapatikana



Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi Dk. Pindi Chana








**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii Balozi Dk. Pindi Chana, amesema Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ili itumike kwa Watanzania wote badala ya nishati chafu ya kupikia ambayo huhatarisha maisha yao na kuharibu mazingira.

Alisema hayo jijini Dodoma juzi wakati akihamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia programu ya Pika Kisasa inayoendeshwa na Wizara ya Nishati.

Alisema Serikali imeandaa mkakati madhubuti wa nishati safi ya kupikia wenye lengo kuwaondoa Watanzania katika adha itokanayo na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Alisema mkakati huo wa nishati safi ya kupikia ni wa miaka 10 ambao unatoa mwongozo wa kufikia lengo la asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Kuhusu suala la utunzaji wa mazingira, alisema asilimia 48 ya eneo la Tanzania ni misitu, hivyo matumizi ya nishati safi ya kupikia yatasaidia uhifadhi wa misitu ili kuwa na uhakika wa mvua.


"Watanzania tupo milioni 61.7 tunaenda milioni 62, kwa idadi hii kubwa tuliyonayo tusipoachana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia, tunaona namna gani tunaenda kuharibu mazingira yetu, hii misitu tunaihitaji, hivyo nishati safi ya kupikia ni muhimu kwa ustawi wa mazingira," alisema.

Alisema matumizi ya kuni na mkaa yamekuwa yakisababisha uharibifu mkubwa kwenye misitu na ndicho chanzo cha upatikanaji wa mvua zisizotabirika.

Alitoa wito kwa jamii kuishi kwenye maono ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuondokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



## Mgao wa umerudi kwa Temeke pekee?

Tunachofahamu ni kwamba kutokana na juhudi kubwa za Rais Samia Suluhu Hassan za kuendeleza uzalishaji wa umeme kupitia Bwawa la Kuzalisha umeme la Julius Nyerere, Tanzania haina tena upungufu wa umeme na hivyo hakuna mgao.

Lakini kwetu Temeke, hususani wakazi wa Mtaa wa Yombo na Msikiti wa Nurulyakini hadi Mwembe Yanga, hali imekuwa ni tofauti. Kila wiki, hususani siku za wikiendi tunakatiwa umeme kwa siku nzima. Hata Jumapili hii hatukuwa na umeme kwa siku nzima. Wakikata saa 12 asubuhi basi jua hapo mpaka usiku. Kwanza wanakata ghafla na hawaelezi sababu. Ndio maana tunauliza, mgao wa umeme umerudi? Kama umerudi kwa nini mtaa wetu pekee?




MAONI YA MHARIRI

## Tushiriki, tuachague viongozi bora kumuezi Mwalimu Nyerere

NCHI yetu inaingia kwenye nyakati muhimu za kupata viongozi kwa ajili ya kutuongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano. Mwaka huu tutakuwa na Uchaguzi wa Serekali za Mitaa na mwaka kesho tutakuwa na Uchaguzi wa Mkuu.

Kwa mantiki hiyo, sisi wananchi tuna mambo kadha wa kadha muhimu ya kufanya. Moja ni kuhakikisha tunajiandikisha, iwe kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura au kuwemo kwenye orodha ya wapiga kura kwa sababu ya uchaguzi wa Serekali za Mitaa kwani hizi ni chaguzi mbili tofauti zikisimamiwa na mamlaka mbili tofauti.

Baada ya kuhakikisha tumejiandikisha, tuna dhima ya kugombea au kushawishi wenzatu ambao tunaona wanafaa kugombea uongozi.

Lakini kubwa ni kuhakikisha tunashiriki kupiga kura kwa sababu kutopiga kura ni kuruhusu watu wengine wakuchagulie kiongozi usiyemtaka! Tusipoteze haki yetu hii muhimu ya kuchagua viongozi au kuchaguliwa.

Kwa bahati nzuri Mwalimu Julius Nyerere ambaye tunaadhimisha miaka 25 tangu alipotuacha, alishatupa miongozo na vigezo vya kuchagua viongozi bora. Mwalimu alikuwa akitutaka tuchague kiongozi anayeguswa na matatizo yetu na anayejua kuwa uongozi ni mzigo.

Mwalimu alituonya tuwaepuka kama ugonjwa wa ukoma wale wanaowania uongoziol huku wakipitapita na kuhonga wapiga kura. Kimsingi Mwalimu Nyerere alikuwa akihumiza kuchagua viongozi waadilifu, waaminifu, wazalendo, wasiojikweza na wasiotoa maamuzi ya kibabe bali huwashirikisha wananchi.

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa bila shaka tunawajua viongozi kadhaa ambao wamekuwa wakitumia madaraka yao kusababisha migogoro ya ardhi ikiwemo kuuza viwanja holela. Hao hawatufai hata kidogo.

Lakini tunapenda pia kutumia wasaa huu kuvihimiza vyama vya siasa kushiriki sawasawa kwenye uchaguzi serikali za mitaa.

Tumeona Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), William Lukuvi akipita akiwahimiza viongozi wa vyama vya siasa juu ya umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Tunaamini vyama vyote 19 vitampokea na vitakuwa tayari kuhamasisha na kushiriki uchaguzi wa amani. Hatutarajii wawe chanzo cha vurugu na uvunjifu wa amani wakati wa chaguzi.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

## Kweli wapinzani wanatapatapa

RAIS Samia Suluhu Hassan amewasihi Watanzania kuwakataa wale wote wanaotaka kuwagawa kwa maslahi yao binafsi, huku akiwasisitiza kutanguliza maslahi mapana ya nchi.

Rais Samia aliyasema hayo hivi karibuni wakati akiwa kwenye ziara yake mjini Songea mkoani Ruvuma. "Niwatake Watanzania kutanguliza maslahi ya nchi kabla ya maslahi binafsi, tuwakatae wote wanaotaka kutugawa kwa sababu za kisiasa au tofauti za kiitikadi, Watanzania ni wamoja, Tanzania ni moja, sisi ni mtu mmoja," alisema Rais Samia.

Dk. Samia hakusita kubainisha ukweli kwamba wanaowagawa Watanzania hivi sasa ni baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani.

Amepasha kuwa, hivi sasa wapinzani wameishiwa hoja na kilichobaki kwao ni kutaka kuivuruga nchi ili isitawalike na hatimaye kuondoa amani na utulivu uliopo.

Rais Dk. Samia ametaka wapinzani wa aina hii wasionewe haya, bali wakemewe kwa nguvu zote ili wasituvurugie amani yetu.

> **Niwatake Watanzania kutanguliza maslahi ya nchi kabla ya maslahi binafsi, tuwakatae wote wanaotaka kutugawa kwa sababu za kisiasa au tofauti za kiitikadi, Watanzania ni wamoja, Tanzania ni moja, sisi ni mtu mmoja**

Kauli hii ya Rais Dk. Samia haiwezi kupita bila kuungwa mkono, ni kweli tangu tulipopata Uhuru mwaka 1961,Watanzania tumekuwa wamoja kwa shida na raha; mshikamano huu umetutawala tangu zama hizo.

Kamwe hatujawahi kuyumbishwa na masuala ya aina yoyote ile yawe ya kisiasa au ya kidini. Hivyo ndivyo alivyotuacha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere ambaye tunaadhimisha miaka 15 ya kuishi bila yeye.

Tuliingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992; hivyo kila mwananchi ana haki, uhuru wa kujiunga na chama chochote cha siasa ili mradi asivunje sheria za nchi.

Kwa mfano, kutoa maneno ya kashfa na kejeli kwa viongozi wa dola au mtu yeyote kwa lengo kuchochea chuki au kuchafua amani iliyopo mahali husika hilo ni kosa la wazi kwa kila mwenye akili timamu.

Siasa za unafiki ni hatari sana. CCM ni chama tawala na kilichopewa ridhaa na wananchi kuunda dola hivyo, haiingii akilini kuwa CCM iwe chanzo cha chokochoko kama wanavyodai baadhi ya viongozi wa upinzani.

Hizo ni siasa muflisi na zenye hoja potofu ambazo zinaweza kuhatarisha amani na utulivu wa nchi. Wananchi wote ni wamoja na wana mshikamano uliokakamaa. Wanaishi pamoja kwenye mitaa au kwenye nyumba za kupanga bila kujali huyo ni shabiki wa Chadema, CUF au CCM.

Siasa za kuviziana au kuchafuana ni hatari kubwa na hazina manufaa yoyote katika jamii na taifa.

Chama chochote cha siasa lengo lake ni kuongoza dola. Hilo linawezekana tu kama chama kina sera na malengo mazuri ambayo yatawavutia wananchi ili wawape ridhaa kwa njia ya kura ili kuongoza dola lakini si kwa blaa blaa na lugha za uchochezi..

# Ujenzi wa barabara ya lami kilomita 104 Iringa-Msembe

## ● Je, tumlaumu Samia na kwa hili au tumpongeze?




**Waziri wa Ujenzi Innocent Bashungwa, akizungumza na wananchi wa Iringa wakati wa utiaji saini ujenzi wa barabara ya lami kilomita 104 Iringa – Msembe**

**Na Francis Godwin, Iringa**

MAENDELEO ni barabara na barabara ni maendeleo.

Kauli hii inaakisi umuhimu wa miundombinu bora ya barabara katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Huwezi kuzungumzia maendeleo bila kuwepo kwa barabara imara.

Ujenzi wa barabara za kiwango cha lami nchini Tanzania, umechochea ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Hafla ya utiaji saini mikataba ya ujenzi wa barabara ya Iringa-Msembe yenye urefu wa kilomita 104, iliyofanyika Septemba 21, mwaka huu, inaashiria mwanzo wa hatua muhimu ya kuimarisha sekta ya utalii na uchumi katika Mkoa wa Iringa na Taifa kwa ujumla.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, alieleza kuwa barabara hii itarahisisha upatikanaji wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, moja ya hifadhi maarufu nchini inayovutia watalii wa ndani na wa nje.

Hifadhi ya Ruaha imekuwa ikikumbwa na changamoto za miundombinu duni, hasa nyakati za mvua, hali inayowazuia watalii wengi kufika hifadhini kwa urahisi.

Ujenzi wa barabara hii ya lami utarahisisha usafiri na hivyo kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi hiyo.

Watalii wa ndani nao watafaidika kwani gharama za usafiri zitapungua na hii itawawezesha Watanzania wengi zaidi kufurahia utalii wa ndani.

Mbali na utalii, barabara ya Iringa-Msembe itachangia kuboresha uchumi wa wakazi wa maeneo yanayozunguka barabara hiyo.

Wakulima wa Iringa wasafirisha mazao yao kama nyanya kwa urahisi zaidi.

Barabara hii itaimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, hivyo kuongeza kipato cha wakulima wadogo na kuchangia katika kupunguza umaskini vijijini.

Kwa upande wa huduma za jamii, barabara ya lami ya Iringa-Msembe, itasaidia katika sekta ya afya na elimu.

Rosemary Nyalusi, mkazi wa Nzihi mkoani Iringa, anaeleza kuwa itakuwa rahisi kwa wakazi kufika katika hospitali na vituo vya afya vilivyopo mjini Iringa na hivyo kuboresha upatikanaji wa huduma za haraka.

Pia, vifaa tiba vitafikishwa kwa urahisi kwenye vituo vya afya vya vijijini.

Sekta ya elimu pia itanufaika kwani wanafunzi watafika shuleni kwa wakati na kwa usalama.

Walimu nao watapata urahisi wa kusafiri kwenda na kutoka shuleni, hali itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa elimu.

Inaendelea uk. 8

# Ujenzi wa barabara ya lami kilomita 104 Iringa-Msembe

Inatoka uk. 7

Haya yote ni mafanikio makubwa yanayotarajiwa kutokana na ujenzi wa barabara hii.

George Kaundama, mmiliki wa hoteli mjini Iringa, anaeleza kuwa ujenzi wa barabara ya Iringa-Msembe, utaleta fursa nyingi za uwekezaji.

Wawekezaji wataanzisha miradi kama hoteli, migahawa na vituo vya mafuta, hali ambayo itachochea maendeleo katika Mkoa wa Iringa.

Pia, uwekezaji katika sekta ya kilimo, utaongezeka kwani barabara itawawezesha wakulima kusafirisha mazao yao kwa urahisi na hivyo kuanzisha viwanda vidogo vya kuchakata mazao kama viazi na mboga.

Said Omari, mtoa huduma za usafiri, anabainisha kuwa barabara hiyo itaongeza ufanisi katika sekta ya usafirishaji.

Kwa sasa, magari yanakabiliwa na changamoto za barabara mbovu, hali inayosababisha ucheleweshaji wa mizigo na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji.

Kwa kujengwa kwa barabara ya lami, usafirishaji wa bidhaa na abiria utaimarika, na hivyo kupunguza gharama za usafiri na kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi.




Mkandarasi na watalamu, wakisaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya lami kilomita 104 kati ya Iringa mjini na Msembe

Kwa upande wa watalii wa ndani kama Michael Sanga, barabara hii itawawezesha kufika hifadhini kwa urahisi, hasa watalii kutoka mikoa ya jirani kama Mbeya, Njombe, na Dodoma.

Barabara hii itachochea ongezeko la watalii na mapato yanayotokana na utalii katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mbunge wa Jimbo la Ismani, Wiliam Lukuvi, anaeleza kuwa wananchi wa jimbo lake wamesubiri kwa hamu kubwa ujenzi wa barabara hiyo. Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ametimiza ahadi ya muda mrefu ya kujenga barabara hiyo, iliyoahidiwa na serikali za awamu zilizopita.

Mbunge wa Kalenga, Jackson Kiswaga na Mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu, pia wamepongeza serikali kwa kuanza ujenzi huo.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, anasema kuwa ujenzi wa barabara hiyo utatoa mchango mkubwa katika sekta ya utalii kwenye Hifadhi ya Ruaha.

Kwa mujibu wa Bashungwa, barabara hii ni sehemu ya mkakati wa serikali wa kuboresha miundombinu ili kufungua fursa za kiuchumi, hasa katika sekta ya utalii na kilimo.

Ujenzi wa barabara ya Iringa-Msembe utagharimu Sh. bilioni 142.56 na itakuwa kiunganishi muhimu kati ya Mkoa wa Iringa na Hifadhi ya Ruaha.

Mradi huu ni sehemu ya mpango wa Serikali ya Awamu ya Sita ya kuboresha miundombinu ili kufungua fursa za kiuchumi, kukuza utalii wa kusini, na kuongeza pato la taifa.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Salim Abri Asas, anaeleza kuwa ujenzi wa barabara hii ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa vitendo.

Anasema barabara hiyo itafungua milango ya fursa nyingi za kiuchumi na kusaidia sekta ya utalii kuvutia watalii zaidi.

Hakuna ubishi kuwa ujenzi wa barabara ya Iringa-Msembe ni hatua muhimu katika juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia za kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi.

Ni ukweli usiopingika kuwa maendeleo ni barabara na barabara ni maendeleo.

Tuwe na moyo wa kushukuru heri kuitwa chawa maendeleo wa kumpongeza Rais Dk. Samia kwa kazi hii nzuri.

**Mwandishi wa Makala haya ni Francis Godwin ni mtayarishaji wa maudhui mitandaoni kupitia Matukio Daima media pia mwandishi wa gazeti hili anapatikana kwa simu 0754026299 email: matukiodaima3@gmail.com**




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Leo yetu ndiyo kesho yetu


Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumatano Oktoba 9-15, 2024 |

UTALII
AFYA
JAMII



Jarida hili haliuzwi

# Msekwa: Mkongwe aliyeshuhudia mengi kwa Mwalimu Nyerere

UK. 12 & 13




# Makubwa yamefanyika miaka 25 bila Nyerere

## ■ Awamu ya Sita yaendelea kumuenzi kwa vitendo

**Na Hamid Yassin**

HAKIKA saa zimepita, siku, wiki, miezi mwaka na sasa ni miaka 25 imepita Tanzania bila kuwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kiongozi aliyesimama kidete kuhakikisha mataifa ya Kusini mwa Afrika yanajikomboa kutoka katika makucha ya wakoloni.

Licha ya Mwalimu Nyerere kutangulia mbele ya haki, fikra na maono yake yataendelea kuishi milele na ndio maana hata Rais wa Awamu ya Sita Dk. Samia Suluhu Hassan anaendeleza mambo mengi ambayo yaliasisiwa na Mwalimu kwa vitendo.

Miongoni mwa misingi thabiti aliotuachia Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ni moyo wa uzalendo baina ya Watanzania pamoja na kuishi bila kubaguana kwa dini, kabila wala ukanda, mambo ambayo nchi nyingi yamewashinda na hatimaye kuingia katika machafuko.

Aidha, kazi kubwa ambayo Mwalimu Nyerere alifanya ambayo imeendelea kuishangaza dunia ni, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliozaa Tanzania ambao ni mfano wa kuigwa duniani kwa kuwa umedumu na unaendelea kudumu bila vikwazo wala kutoelewana kokote.

Mwalimu Nyerere pia ni mwasisi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa kushirikiana na wakuu wengine wastaafu wa mataifa ya Afrika Mashariki, na pia Jumuiya ya Uchumi Kusini mwa Afrika SADC ni kazi za mikono yake ndio maana heshima yake sio tu kitaifa bali hata kimataifa. Japo EAC iliwahi kuvunjika, lakini viongozi waliokuja baadaye waliona umuhimu wa kuifufua na sasa inaendelea kuchanja mbunga.

Vita inayopiganwa sasa ya kukuza uchumi kupitia kukusanya kodi kwa njia sahihi na kudhibiti rushwa, ni miongoni mwa mambo ambayo Mwalimu Nyerere aliyavalia njuga ambapo katika kipindi chake suala la kujilimbikizia mali ama suala la ufisadi ilikuwa misamiati ambayo hakutaka kuisikia.

Kwa kuwa tumeshuhudia jinsi Rais wa Awamu ya Sita anavyofuata nyayo za Mwalimu Nyerere ni wazi haya maendeleo makubwa yanayopatikana tena kwa kipindi hiki kifupi cha miaka yake mitatu na nusu, mfano kuendeleza ujenzi wa mradi mkubwa wa Umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji pia lilikuwa ni wazo la Mwalimu Nyerere.

Ndoto za Mwalimu Nyerere pia zimeendelea kutimizwa na Serikali ya Awamu ya Sita kuhakikisha inajenga vituo vya afya kila mahala, hospitali za wilaya pamoja na zile za rufaa za mikoa ambapo tunashuhudia ukuaji wa sekta hii kila uchao.

Mambo yanayowezekana na yanayofanyika kwa sasa ni kutokana na Watanzania kuamua kwa dhati kulipa kodi na kuamua kufanya kazi, Serikali iliyopo madarakani sasa inamuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo kwani aliasisi mambo mengi ambayo nchi inajivunia.

Miaka 25 bila kuwepo Mwalimu Nyerere ukuaji wa uchumi umeendelea kuimarika sambamba na kuboreshwa kwa huduma muhimu za jamii, kwa sasa kuna vijiji 12,423 Tanzania nzima. Ukienda kijiji kama cha Kurwaki, Musoma vijijini mkoani Mara, wakati Mwalimu anaondoka duniani, asilimia zaidi ya 95 ya nyumba zilikuwa za nyasi lakini leo 2024, hakuna nyumba ya nyasi, labda baadhi ya vyoo na jiko. Kwa upande wa Tanzania Bara kuna vijiji 12,319, vitongoji 64,384 na mitaa 4,263.

Ukuaji wa vijiji miji na mitaa umeenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu pamoja na kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za msingi ikiwemo elimu, afya, maji pamoja na umeme wa uhakika hasa maeneo ya vijijini kupitia mradi wa REA.

Miaka 25 bila Mwalimu Nyerere hata idadi ya Watanzania imeongezeka ambapo kwa sasa wako takribani watu milioni 61.7 kwa uwiano ambao vijana ndio wengi zaidi, na kwa kutambua umuhimu wa vijana katika Taifa lolote Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kwa makusudi kusimamia sera ya viwanda baada ya kufufuliwa kwa viwanda ambavyo viliasisiwa katika kipindi cha Baba wa Taifa. Serikali pia imewapeleka kwenye kilimo vijana kupitia mpango wa jenga kesho iliyo bora (BBT) na hata imeboresha mitaala ili kuwawezesha vijana wanapomaliza elimu zao kabla ya kujiunga na vyuo vya kati na vikuu wawe tayari wana ujuzi wa kuajiriwa au kujiajiri.

Pia uwekezaji umekua kwa kiasi kikubwa na sasa madini yameanza kuiletea nchi neema baada ya kukaa ardhini kwa muda mrefu. Ikumbukwe kwamba kipindi cha Mwalimu Nyerere alikemea kwamba kama uwezo wa kuchimba madini hatuna tusubiri hadi tutakapopata uwezo na teknolojia ya kuyachimba, sasa uwezo upo na usimamizi thabiti upo hivyo moja ya ndoto za Mwalimu Nyerere zimefanyiwa kazi vizuri.

Kwa kuwa idadi kubwa ya vijana hasa wa kizazi cha sasa, hawajui mema mengi na maono mengi aliyokuwa nayo Baba wa Taifa ni wakati mwafaka sasa, kwa wasomi na wanasiasa kutumia muda mwingi kuwaelezea vijana mambo mengi yaliyoasisiwa na Mwalimu Nyerere lakini pia mchango wake uliotukuka katika amani, mshikamano na uhuru wa mataifa mbalimbali duniani.

Kuwa kijana wa chama fulani hakufanyi au kumzuia kijana husika kutumia ufahamu wake vizuri kwa manufaa ya nchi yake. Hii ndio maana ya kijana kuwa ni jeuri ya chama na ya jeshi kubwa. Hii ndio maana ya kijana kuwa tija na mtaji kwa taifa.

Msemo huu haumaanishi kijana kuimba nyimbo za 'iyena iyena' tu japo ni muhimu, au kushindana kuvaa sare na magwanda ya chama, muhimu zaidi ni kwa kijana kutoa mchango wake wa fikra kwa manufaa ya nchi yake ikiwemo kuibua changamoto na kuleta hoja mpya zinazoweza kulisukuma taifa hatua kadhaa mbele.

Nimefuatilia mno mahala pengi, vijana wengi wameathiriwa sana na aina ya vyama vyao wanavyotoka na hivyo hawatumii vyema ufahamu wao kwenye masuala ya kitaifa, vijana wengi wanapenda sana mapambio na vigelegele huku wengine wakipinga na kuponda kila jambo linalofanywa na serikali.

Unaweza kukuta vijana wote wa CCM wanashangilia kitu kimoja wakati wale wa upinzani nao wakikesha mitandaoni kupinga na kuponda jambo lolote linalofanyika ndani ya nchi.

Sasa imeshakuwa mazoea na inafahamika wazi kwamba kijana wa upande fulani ni maalumu kwa kusifu na kijana wa upande mwingine ni maalumu kwa kupinga, yaani kama sera za Usimba na Uyanga. Hii si sawa.

Tujikumbushe suala la kikokotoo. Vijana na wabunge wengi wa CCM walipiga mapambio na kusifu sana suala hilo mpaka Rais alipokuja kuweka sawa jambo hilo kwa kusema hii si sawa na kuagiza muswada ule upitiwe upya.

Upande wa upinzani kila uchao wanapinga yanayofanywa na serikali ikiwemo ununuzi wa ndege, ujenzi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere na mengine ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo mwanzoni waliipinga sana. Yaani hakuna fikra mbadala kwa vijana wengi. Ni kusifu ama kupinga.

Haya mapambio ya ndio mzee hayafai, yamepitwa na wakati. Kupinga kila jambo pia ni kukosa uzalendo na tabia za mtu mchawi na mnafiki. Ni wakati wa vijana kujipambanua na kutumia ufahamu wetu vizuri kwa manufaa ya nchi.

Kijana unakuwa mzalendo na mtaji kwa taifa kwa namna unavyoweza kuleta fikra mpya na mbadala zinazoweza kulisaidia taifa kusonga mbele.

Ni wajibu kwa kijana yeyote bila kujali upande wake wa kiitikadi kuibua hoja, ushauri na mawazo kwa namna nzuri kwenda kwa wenye mamlaka na viongozi wetu ili kulisaidia taifa hili.

Miaka 25 bila Mwalimu Nyerere mambo mengi yanatekelezwa ambayo aliyawaza na alitamani yafanyike, katika kipindi hiki cha kumbukumbu yake ni vyema Watanzania watafakari jinsi njema ya kumuenzi sio tu kwa kufanya kazi kwa bidii lakini pia kuyaenzi yale ambayo aliyaamini.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*

# Tumuenzi Mwalimu Julius Nyerere kwa kuchagua viongozi bora

**Na Hamid Yassin**

NI miaka 25 sasa tangu Watanzania tuondokewe na mwasisi wa Taifa hili, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika kipindi chote hicho Watanzania tunaendelea kumkumbuka kwa maono aliyokuwa nayo juu ya nchi yetu lakini pia uhitaji wa kiongozi mzalendo, mwadilifu na mwenye utayari wa kuleta maendeleo kwa watu wake ili kukidhi matarajio yao.

Nenda uendako Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mahriri na shupavu, mwenye maoni na mwadilifu. Miongoni mwa hotuba zake maarufu ni ile aliyoitoa mkoani Mbeya katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Mei Mosi, 1995 yaliyofanyika kwenye uwanja wa Sokoine.

Hotuba hiyo aliitoa wakati Tanzania ikijhiandaa kufanya uchaguzi mkuu katika mfumo wa vyama vingi vya kisiasa nchini kwa mara yua kwanza.

Pamoja na kwamba Mwalimu alizungumzia masuala ya wafanyakazi, maendeleo na kukemea dosari zilizoanza kujitokeza nchini, kwa hisia pia alisisitiza wajibu wa viongozi wanaochaguliwa (kuanzia ngazi ya diwani, mbunge hadi rais) wawe ni wenye uwezo katika kutatua matatizo ya jamii zao.

Katika hotuba hiyo, Mwalimu alisema, "Tunataka mtu anayetaka kuwa rais wetu ajiulize anataka kuifanyia nini nchi yetu na sio nchi yetu itamfanyia nini?" swali alilomtaka kila anayetaka kuwa mgombea wa chama chochote kujiuliza kwa dhati kabisa.

Aidha, Mwalimu alitanabaisha kuwa, mgombea atakayechaguliwa akerwe na hali ya umasikini wa Watanzania na kwamba kero hiyo imsukume kuwa tayari kuishughulikia, iwe ni katika ngazi ya udiwani, ubunge na urais.

Vilevile, alionya wagombea kuwa Ikulu si mahali pa kukimbilia isipokuwa ni mahali ambapo unakutana na matatizo mengi ya wananchi kama vile njaa, umaskini na huna budi kuyatatua matatizo hayo kwa manufaa ya taifa zima.

"Ukiona mtu anapakimbilia, na hasa anapotumia vipesa kwenda Ikulu mtu huyo ni wa kuogopa kama ukoma! Mtanzania wa leo hawezi kununua watu bila kwanza yeye kununuliwa, na kama kanunuliwa atataka kuzilipaje, … kama kakopa atazirudishaje?" Alihoji Mwalimu.

Naam; hayo yalikuwa maneno 'Kuntu' ya hayati Mwalimu Nyerere kuelekea Uchaguzi Mkuu wa kwanza wa vyama vingi kufuatia kurejeshwa kwake mfumo huo mwaka 1992 hapa nchini.

Tunapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba mwaka huu na ule mkuu mwakani Oktoba, ndiyo wakati wa kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kuchagua viongozi bora na si bora viongozi! Tuepuke wagombea wanaokimbilia uongozi wakati kimsingi uongozi ni mzigo na mtu makini kabisa kabisa haukumbilii.

Kwa upande wa Uchaguzi Mkuu mwakani, kwa mtazamo wangu hakutakuwa na taabu, kwani Rais wetu wa sasa, Dk. Samia Suluhu Hassan ameshathibitisha kwa vitendo kuwa, amekidhi vigezo vyote vya kiongozi tunayemtaka. Kilichobaki ni kuomba uhai tu ili mwakani tumrejeshe Ikulu kupitia sanduku la kura.

Kazi ipo huku kuanzia uchaguzi huu wa Novemba mwa huu wa Serikali za Mitaa na zile za madiwani na wabunge mwakani, ambako tutatakiwa kutumia hekima alizozitaja Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere katika kuwapata wagombea bora.

Bado tunakumbuka namna Mwalimu Nyerere alivyoipenda nchi yake, alijitoa kwa nadharia na vitendo, alikuwa mshauri katika masuala mbalimbali kuanzia siasa, uchumi, na hata masuala ya kijamii.

Mwalimu aliipenda nchi yake na alikuwa tayari kusaidiana na viongozi wengine wanaoijenga nchi bila kujali itikadi za kisiasa au kidini.

Alikuwa kiongozi mkweli asiyetetereka kwani alikuwa tayari kuwapinga na kuwakemea bila woga viongozi walioharibu nchi hata kama walitoka katika chama chake.

Alitamani kuona taifa linaongozwa na kiongozi mwadilifu, jasiri na shujaa, kiongozi mwenye nia ya dhati ya kupambana na maadui ujinga, maradhi na njaa ili kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa watu.

Kupitia hotuba zake, ni kama vile Baba wa Taifa aliota ndoto juu ya Rais wa Awamu ya Sita, Dk. Samia.

Miaka mitatu iliyopita Watanzania tulishuhudia Katiba yetu ikitupatia Rais wa Awamu hii kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Dk. John Pombe Magufuli. Tangu alipoapishwa rasmi, Machi 19 mwaka 2021, Rais Dk. Samia amedhihirisha kwa vitendo kuwa ile ndoto ya Baba wa Taifa katika hotuba yake ya Mei Mosi, 1995 imetimia kwa kuwa tuna kiongozi anayeguswa na masilahi ya taifa na Watanzania kwa ujumla, sifa ambayo Baba wa Taifa alikuwa akisisitiza.


Katika hotuba yake ya kwanza aliyoitoa Bungeni Jijini Dodoma, Aprili 22, mwaka 2021, Rais Samia aliyataja maeneo yaliyolalamikiwa na wananchi tangu akiwa Makamu wa Rais kuwa ni pamoja na rushwa, ubadhirifu, urasimu, upotevu wa mapato, uzembe sehemu za kazi na migogoro ya wakulima na wafugaji.

Maeneo mengine alisema ni ukosefu wa huduma muhimu za kijamii kama vile maji, nishati, afya, elimu, ajira na ubovu wa miundombinu.

Aidha, Rais Dk. Samia aliahidi kushughulikia matatizo ya wananchi bila kujali itikadi za vyama vya siasa isipokuwa kutanguliza nchi mbele kwa kuwa matarajio na matumaini ya wananchi katika kipindi cha uongozi wake ni makubwa.

"Wanachotaka kuona wananchi ni nchi yetu kupiga hatua kubwa za maendeleo zitakazojibu matumaini yao na kutatua shida na kero zao. Nyie na mimi baada ya uongozi wangu kwisha tutapimwa kwa namna tutakavyokuwa tumetekeleza mambo ambayo tumewaahidi Watanzania wenzetu," alisema Rais Dk. Samia.

Wakati tunaenzi mawazo na nasaha za Baba wa Taifa baada ya miaka 25 tangu alipofariki, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia imefanikiwa kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi kwa kipindi hiki kifupi.



Aidha, serikali imeimarisha nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma, imeondoa urasimu na hivyo kupunguza rushwa kwa kiasi kikubwa ndani ya Serikali na kuongeza ukusanyaji wa kodi kutoka trilioni 1.2 kwa mwezi mwaka 2020 hadi trilioni 3 kwa mwezi kwa mujibu wa makusanyo ya Septemba mwaka huu 2024.

Kwa upande wa kilimo, Serikali ya Awamu ya Sita, imeimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na kuimarisha vyama vya ushirika ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

Kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuanzia Aprili mwaka 2021 hadi sasa vijiji vyote 12,268 nchini vimepatiwa umeme huo, yaani asilimia 100! Na sasa REA wameanza kazi ya kwenda Vitongojini.

Aidha, sekta ya afya imeimarishwa ambapo upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na huduma za matibabu zimekuwa za uhakika ikiwa ni pamoja na kujenga na kukarabati vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za Rufaa na za Kanda pamoja na kuongeza huduma za kibingwa ambazo hapo awali zilikuwa zinapatikana nje ya nchi.

Hatua nyingine zilizochukuliwa katika kuwaletea maendeleo wananchi wa kada mbalimbali ni pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu, sekta ya usafiri na usafirishaji, uanzishwaji wa masoko ya madini, utoaji wa risiti za kielektroniki.

Vilevile, katika Awamu hii, tumeshuhudia Wizara na Idara zote za Serikali zikikamilisha zoezi la kuhamia Dodoma ikiwa mwendelezo aliouacha hayati, Dk. Magufuli na ndoto za Mwalimu Nyerere.

Ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa Bonde la Rufiji wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 unaoendelea kwa gharama ya shilingi trilioni 6.5 tayari vinu vitatu kati ya tisa vilivyopo vyenye uwezo za kuzalisha megawati 705 vinaingiza umeme kwenye gridi ya taifa.

Huku mpaka kufikia Februari mwaka huu vinu vingine vitano vilikuwa kwenye majaribio ya kuzalisha umeme na mafanikio yalikuwa makubwa kwa asalimia zaidi ya 80.

Ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambao gharama zake zimepanda kutoka shilingi trilioni 7 mradi ulipoanza wakati wa Awamu ya Tano hadi shilingi trilioni 24 hivi sasa, tayari usafiri kati ya Dar es Salaam, Morogoro hadi Dodoma umeanza tangu Julai mwaka huu.

Huku maeneo mengine ya ujenzi huo wa Reli ya SGR kulekea Singida, Tabora, Kigoma na Mwanza makandarasi wako kazini na unaendelea kasi ya kuridhisha.

Aidha, viwanda zaidi ya 11,877 vikiwemo vidogo, vikubwa na vya kati vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mafanikio haya yanatokana na ujasiri wa Rais Dk. Samia kufanya maamuzi magumu ambayo yalisuasua huko nyuma lakini sasa yametekelezeka kwa ufanisi ikiwa ni ishara ya kumuenzi Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Nyerere.

Tunapoadhimisha miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, tunayo sababu ya kujivunia mafanikio yaliyopatikana sasa nchini kwa kuwa ndoto ya Baba wa Taifa ya mwaka 1995 inatimia, Watanzania tunaiishi kwa vitendo hasa tunapoangalia hatua kubwa za maendeleo ambazo nchi yetu imezipiga kwa muda mfupi. Ni hali halisi. Lakini ili mambo yawe mazuri zaidi ni lazima tumpe rahisi viongozi makini wa kumsaidia kazi kupitia chaguzi hizi mbili; hii ya mwaka huu ya serikali za mitaa na ijayo ya kupata wabunge. Kutokana na wabunge, Rais pia atapata mawaziri wa kumsaidia.

*Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122020.*

# Msekwa: Mkongwe aliyeshuhudia mengi kwa Mwalimu Nyerere

- Alikuwa anapata ugumu kutoa baadhi ya maamuzi
- Alibarikiwa karama za uongozi, macho yanayoogofya
- Hakujikweza, hakumiliki gari wala nyumba ya maana
- Kuporomoka kwa maadili kulimudhi Nyerere

**Na Hamisi Kibari**



Ni miaka kadhasaa imepita tangu nilipobahatika kufanya mazungumzo na Mzee Pius Msekwa, pale nyumbani kwake Msasani, Dar es Salaam.

Kwangu ilikuwa ni mara ya kwanza kuwa karibu kabisa na hata kuzungumza pamoja na kushikana mkono na mkongwe huyu wa siasa lakini wakati akitukaribisha tukuwa na waandishi wengine nikagundua ukarimu mkubwa alionao, uchangamfu na utani.

Tulikwenda kumwona Msekwa lengo kubwa ni kusikia kutoka kwake namna anavyomzungumzia Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kiongozi ambaye alifanya naye kazi kwa kwa karibu.

**KUKUTANA NA MWALIMU NYERERE**

Mzee Msekwa, akijibu swali lililotaka kujua ni wapi na jinsi alivyokutana na Mwalimu Nyerere kwa mara ya kwanza ambapo alisema walikutana naye Pugu Sekondari, wakati yeye akiwa mwanafunzi, na Baba wa Taifa akiwa mwalimu wake wa somo la Historia.

"Kwa hiyo kukutana kwangu na Mwalimu Nyerere kwa mara ya kwanza, ni darasani katika Sekondari ya Pugu akiwa mwalimu wangu. Huo ulikuwa mwaka 1953, wakati huo ndio Mwalimu akiwa ametoka masomoni, (Chuo Kikuu cha) Edinburgh, (Scotland)," anasema.

Anasema Mwalimu Nyerere, ambaye alikuwa anafundisha somo la Historia ambalo lilijielekeza katika kuwafundisha wanafunzi historia ya Uingereza huku ikiitukuza nchi hiyo, alionekana waziwazi kukerwa na kutofurahishwa na anacholazimika kufundisha.

Mzee Msekwa anasema baada ya kuwa na Mwalimu Pugu, kama mtu na mwanafunzi wake kwa miaka miwili, baadaye alikwenda kusoma Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Aliporejea ndipo akakutana na Mwalimu Nyerere kwa mara ya pili bungeni.

"Nilipotoka masomoni, niliajiriwa kama Katibu Msaidizi wa Bunge jijini Dar es Salaam na kukutana tena na Mwalimu, yeye akiwa ni mbunge (wa kuchaguliwa wa Jimbo la Mashariki)," anasema na kwamba Katibu wa Bunge wakati huo alikuwa Mzungu akiitwa Geofrey Hucks.

Mzee Msekwa anasema alizidi kuwa karibu zaidi na Mwalimu Nyerere wakati alipomtoa bungeni mwaka 1967 lilipotangazwa Azimio la Arusha na kumfanya kuwa Katibu Mkuu wa chama tawala wakati huo, Tanganyika African National Union (Tanu).

"Kwa hiyo hapa utaona tulikuwa mtu na bosi wake, yeye mwenyekiti wa chama, mimi katibu mkuu," anasema.

Anasema pia Mwalimu Nyerere alimteua kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipoanzishwa rasmi mwaka 1970 huku Mwalimu akibaki kuwa mkuu wa chuo hicho, hatua ambayo ilizidi pia kuwaweka karibu kwa sababu alikuwa analizimika kuripoti kwake kila wakati kunapokuwa na haja.

"Nakumbuka wosia alionipa. Aliniambia "Pius, unakwenda kuongoza vijana ingawa na wewe bado kijana. Wanaweza wakalipuka wakati wowote kutokana na kosa la uamuzi utakalolifanya. Sasa ninakwambia hivi, kabla hujafanya uamuzi, jiridhishe kwamba uamuzi huo ukipingwa na vijana uwe na uwezo wa kuutetea na waridhike kwamba ulikuwa ni uamuzi wa busara. Kama utakuwa na mashaka ya jambo unalotaka kuamua njoo kwangu nikusaidie," anasema.

**KARAMA ZA MWALIMU**

Akijibu swali kuhusu inavyoelezwa na wengi kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa ni mtu anayetisha hata kwa viongozi waliokuwa karibu naye, Mzee Msekwa anajibu.

"Ni kweli, kwa mwonekano wake yeye ni kweli. Alikuwa amejaaliwa kipawa kwamba hulka yake ukimtazama unakuwa tayari kumsikiliza anachosema. Siyo kwamba alikuwa anatisha, neno 'kutisha' halipendezi, lakini alikuwa mtu

ambaye anakarama za uongozi.

"Na wengine wamesema, hata mawaziri kwamba ukiitwa na Mwalimu, akikutazama hivi, unanywea na kuwa na wasiwasi hata kama anakuitia jambo zuri," anasema.

Mzee Msekwa anasimulia kisa cha mbunge mmoja wa Kwimba ambaye alivyosikia anaitwa na Mwalimu Nyerere, tena aliyempelekea wito akiwa ni Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, alijificha kwa hofu akidhani amekuja kukamatwa.

Lakini baadaye mbunge huyo alipogundua kwamba huenda hakuna baya analoitiwa akajitokeza. Kesho yake, akapanda ndege kuja Dar es Salaam na kutangazwa kuwa naibu waziri na mke wake aliyeshirikiana naye kujificha akidhani anakamatwa, akashangilia.

"Kwa hiyo utaona kuna hulka za watu zinatisha ama kwa vyeo vyao au sura zao. Mwalimu alikuwa hivyo," anasema Mzee Msekwa.

## MWALIMU NA MAAMUZI MAGUMU

Mzee Msekwa anasema kwamba kutokana na ukaribu wake na Mwalimu, alikuwa anamwona akikumbana na wakati mgumu katika kutoa maamuzi katika baadhi ya mambo fulanifulani yaliyokuwa yanaikabili nchi au dunia.

Anasema mambo ya namna hiyo yako mengi, lakini moja wapo ni pale Ian Smith alipojitangazia Uhuru wa Rhodesia (sasa Zimbabwe) kutoka Uingereza mwaka 1965. Anasema Mwalimu alipopata habari, aliumia sana na sura yake ikabadilika akiwaza afanye nini katika hali hiyo.

Anasema Mwalimu alikuwa akiwaza kama ni mwafaka kukata uhusiano mara moja na Uingireza iliyoonekana kubariki hali hiyo kwa kuwa Rhodesia lilikuwa koloni lake au la.

"Alivyoletewa habari hiyo nilikuwepo, nadhani, kama sikosei nilikuwa nimempelekea miswada ya kusaini ya Bunge, wakati huo nikiwa Katibu wa Bunge. Mwalimu alionekana ameumia sana kwa mawazo. Ikabidi niage niondoke."

Mzee Msekwa anasema Mwalimu alilazimika kumshawishi aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) sasa Umoja wa Afrika (AU) ambao ulikuwa na miaka michache tangu kuanzishwa, Haile Selassie wa Ethiopia, ili aitishe mkutano wa dharura kujadili suala hilo katika kutafuta msimamo wa pamoja.


Anasema Mwalimu Nyerere hakwenda kwenye kikao hicho na badala yake akamtuma Raishid Kawawa. Mkutano uliazimia kwamba endapo Uingereza haitamwondoa kibaraka Smith madarakani ifikapo Desemba 14, basi Afrika ingekata uhusiano na Uingereza.

"Mwalimu hakutaka kuchelewa. Ilipofika Desemba 14 akasimama pale Lumumba katika ofisi za Tanu, akasema Afrika imeamua tukate uhusiano na Uingereza na mimi siwezi kuchelewa, ikifika saa sita usiku (kama watakuwa hawajatekeleza azimio la OAU) mimi sina uhusiano tena na Uingereza."

Anasema mfano mwingine wa ugumu wa maamuzi uliyompata Mwalimu ni kuvuka mpaka hadi Uganda baada ya kumfukuza Nduli Iddi Amin katika ardhi ya Tanzania.

"Baada ya kumfukuza Amini, majeshi yetu yakawa pale mpakani kuzuia majeshi ya Uganda yasije yakaingia tena. Na majeshi ya Uganda nayo yako pale mpakani yakisubiri amri ya kuingia (kuvamia tena). Sasa Jenerali David Musuguri (aliyekuwa mkuu wa majeshi wakati huo) anamwambia Mwalimu, tutakaa hapa muda gani tunatazamana? Tutakaa miaka miwili, mitatu kila mmoja anangoja amri ya kuingia? Hali hii haikubaliki kijeshi. Wewe toa amri twenda hadi Kampala tummalize huyu.

"Mwalimu akamuuliza, mnaweza? Akajibu tunaweza. Yaani hapo Musuguri na wenzake wamemtaka amwambie Mwalimu atoe amri waingie Uganda, wanaona hawawezi kukaa hapo mpakani mwaka mzima wanacheza cheza tu."



Anasema kabla ya kutoa uamuzi, Mwalimu aliwasiliana na marais wenzake aliokuwa nao karibu kuhusu ushauri huo wa majeshi yake.

"Wale wanamjibu kwamba, sasa Mwalimu, si umeshamfukuza? Sasa unakwenda Uganda kufanya nini? Ukifanya hivyo nawe utakuwa mvamizi na sisi hatutakuunga mkono katika hili," anasema.

Anasema jambo hilo lilimwacha Mwalimu katika wakati mgumu wa kuamua afanye nini. Je, awasikilize marais wenzake au majeshi yake? Ilimsumbua... ilimsumbua sana. Siku anatoa uamuzi, na mimi nilikuwepo pale tukiwa na makamu wa Rais, Aboud Jumbe, akaeleza jinsi anavyotaka atekeleza ushauri wa jeshi lake lakini hataki kuwaudhi marais wenzake," anasema.

Mzee Msekwa anasema kwa ajili hiyo, Mwalimu akamtuma Jumbe apande ndege kesho yake aende kuwaambia wanajeshi waache mpango wa kuingia Uganda kutokana na mtazamo wa Afrika huku akiweka wazi kwamba inamuuma sana yeye mwenyewe kwenda kuwazuia vijana wasiingie Uganda.

Anasema wakati Aboud Jumbe akiwa ndani ya ndege kuelekea Bukoba, Mwalimu akabadili mawazo. Akaona hawezi kuwaudhi vijana wake. Akamwambia Katibu wake apige simu kwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera pale Jumbe atakapofika amwambie asiende kufanya aliyomtuma, badala yake kazi hiyo ataifanya mwenyewe.

"Unaona magumu ya kufanya uamuzi. Kumbe uamuzi aliokuwa ameufanya jana ulikuwa umemuumiza sana, usiku wake akabadili mawazo. Akaona hapana, sasa nitawaruhusu vijana wangu waende Kampala. Na hilo akataka alifanye mwenyewe, kwa hiyo akapande ndege akaenda.

"Sarakikya anasema mkutano huo ulikuwa mzuri sana. Wanajeshi walishangilia, wakatamani hata kumbeba Mwalimu kwa sababu ndicho walikuwa wanakitaka. Hawakutaka kusubiri, usiku uleule wakavuka mpaka kuingia Uganda kwa sababu walishajiandaa. Kwa hiyo ilikuwa ni truu turuu mpaka Kampala," anasema.

Mzee Msekwa anasema mfano mwingine kati ya mingi ambayo ilimpa ugumu Mwalimu kuhusu hatua za kuchukua ni pale Oscar Kambona, alipojiuzulu uwaziri pamoja na ukatibu mkuu wa Tanu.

Anasema Kambona mbaye hakupenda Azimio la Arusha, alitoa tangazo la kujiuzulu bila kumshirikisha bosi wake, Mwalimu, huku akiwa ameandamana na waziri mwingine aliyekuwa rafiki yake wa karibu, Kassim Hanga. Mzee Msekwa anasema alihudhuria katika kikao hicho cha Kambona, ambacho hata hivyo hakusema sababu za kujiuzulu.

"Nilimwona dhahiri Mwalimu amehuzunishwa sana na kitendo hicho akifikiri achukue hatua gani. Aliona kana kwamba Kambona ni waziri na katibu mkuu wa chama halafu amechukua hatua hiyo bila kumshirikisha. Je, ni hujuma? Niliona ilimpa wakati mgumu sana," anasema.

## MWALIMU MCHEKESHAJI, MCHESHI

Mzee Msekwa anasema Mwalimu alikuwa mcheshi na mchekeshaji sana ukimkuta akiwa na furaha. Anasema alikuwa anawapigia hadithi mbalimbali zikiwemo zilizomhusu yeye mwenyewe Mwalimu.

"Alikuwa anapiga hadithi. Kwa mfano kuna hii iliyohusu jinsi alivyoozwa mwanamke kwa mila za Kizanaki ambaye yeye hakua anampenda, lakini akakaa kule kwa mama yake… alikuwa akihadithia vitu kama hivyo," anasema.

## KUPOROMOKA KWA MAADILI

Mzee Msekwa anasema, hata kabla hajafariki dunia, moja ya kitu kilichomsononesha sana Mwalimu Nyerere ni kuporomoka kwa maadili. Mzee Msekwa alisema hilo wakati akijibu swali lililotaka kujua jambo ambalo anadhani Mwalimu angetokea leo lingemsikitisha.

"Wala usiende kwenye kutokea leo. Alionesha kutofurahi kwake angali akiwa hai; suala la maadili. Alisema ya moyoni kwenye hotuba yake ya Mei Mosi pale Mbeya. Kwa kukariri maneno yake Mwalimu alisema: 'Tulikuwa na Azimio la Arusha, wamekwenda Zanzibar wamefuta hilo Azimio la Arusha, hakuna nchi ambayo haina miiko ya uongozi, Marekani wanayo, Japan wanayo…' Ni hotuba yake ambayo huwa inarudiwa mara kwa mara," anasema.

Anasema lingine lililomuudhi Mwalimu angali akiwa hai ni suala la kuchezea Katiba hasa pale Zanzibar ilipotaka kujiunga na Jumuiya ya Nchi za Kiislamu (OIC).

"Mwalimu alikuwa si mtu wa kufichaficha. Akiona jambo limekaa vibaya analisema palepale," anasema.

## NYERERE SI MTU WA KUJIKWEZA

Mzee Msekwa anasema Mwalimu Nyerere hakuwa mtu wa kujikweza wala kupenda mali na alikuwa kiigizo kizuri kwa viongozi wengi waliofanya kazi naye akiwemo yeye (Msekwa).

"Mwalimu Nyerere hakupenda mali. Hakuwahi kuwa na gari yake binafsi, yaani hakuwahi kununua gari. Hakuwahi hata kujifunza udereva. Hakuwahi kuwa na nyumba (ya maana kule kijijini Butiama) ingawa alikuwa anakwenda mara kwa mara akiwa rais.

"Kuna kanyumba alikokuwa anafikia, ni kale alikokajenga wakati anajiandaa kuoa. Si unajua kimila kule ukitaka kuoa mke lazima uwe na nyumba, basi akajenga kanyumba ka vyumba viwili. Kwa hiyo ametumia kanyumba hako wakati wote urais wake (miaka 23) kila anapokwenda mapumziko Butiama."

Mzee Msekwa anasema wakati Mwalimu Nyerere alipotangaza kustaafu, ndipo chama kikaamua kumjengea nyumba Butiama.

"Mimi ndiye nilitumwa na chama kwenda kumwambia Mwalimu kwamba kama zawadi yako, chama kimeamua kukujengea nyumba. Akasema 'ninashukuru'. Hilo hakubisha, alisema ninashukuru.

"Yaani nyumba yenye hadhi kidogo tumemjengea sisi katika chama wakati anastaafu. Na mimi ndiye nilikwenda kumkabidhi hiyo nyumba baada ya kukamilika," anasema.

Mzee Msekwa anasema kama chama kisingeamua kumjengea nyumba, Mwalimu angerudi kijijini baada ya kustaafu urais na kufikia kwenye nyumba yake ya vyumba viwili.

## KUTAKA KUONDOKA MADARAKANI MWAKA 1980

Mzee Msekwa anasema Mwalimu awali alikuwa amepanga kung'tuka mwaka 1980 akimaanisha kwamba asingeshiriki uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

Lakini kutokana na matatizo ya kiuchumi, na hasa kwa vile nchi ilikuwa imetoka kwenye vita vya Kagera dhidi ya Nduli Iddi Amin akashindwa kuondoka madarakani.

"Kama mnakumbuka hiki ndicho kipindi cha kujipanga kwenye mistari ukitaka kununua sukari au mahitaji mengine. Mwalimu akasema nikiondoka sasa watasema amekimbia matatizo na kumwachia mwingine. Ngoja nipambane nayo mwenyewe. Hicho ndicho kilichombakisha kwenye urais," anasema.

# Alianza JPM, Samia anakamilisha Dodoma aliyoitaka Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

KUMBUKUMBU mbalimbali za kihistoria zilizopo zinaonesha kwamba hadi mwaka 1948, Dodoma ilikuwa ni mji mdogo, wakati huo ukiwa na watu wazima takribani 3,458.

Lakini sensa iliyofanyika miaka minne baadaye ilionesha kukuwepo kwa Waafrika 9,375 Dodoma, Wahindi 2,113, Wazungu 360, Waarabu 311 na Wasomali 58.Licha ya kuwa na idadi ndogo ya watu, mji wa Dodoma uliendelea kukua hadi kufikia kuwa mji wa kibiashara na mwaka 1952 Dodoma ilikuwa na watu 12,217.

Miaka 15 baadaye, watu waliongezeka mara dufu na kufikia jumla ya watu 23,559 kwa mujibu wa hesabu iliyofanywa mwaka 1967. Tangu wakati huo mji wa Dodoma umekuwa na ongezeko la watu mwaka hadi mwaka. Katika sensa ya mwaka 2022, idadi ya wakazi wa Mkoa wa Dodoma ilihesabiwa kuwa 3,085,625.

Inaelezwa kwamba wazo la kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya Tanzania lilikuwepo tangu mwaka 1915 wakati wa uawala wa kikoloni lakini faida za Dar es Salaam kama bandari ya kidola zilipewa kipaumbele zaidi.

Fikra za kufanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi ilifanywa kama shauri maalumu kufuatia mjadala wa wabunge waliochaguliwa na wananchi mwaka 1959.

Mjadala huo ulitengewa siku mbili kwa ajili ya kujadili uhamisho wa makao makuu sambamba na kujadili ubora wa sehemu mbalimbali.

Hata hivyo, kila mjumbe alionesha kupendekeza sehemu aliyotoka iwe ndio makao makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kulikoonekana ni pembezoni mwa nchi na miongoni mwa miji iliyopendekezwa ni Iringa, Tabora, Arusha na Dodoma.

Lakini baadhi ya wajumbe waliotaka Dodoma iwe makao makuu ya nchi kutokana na kuwa katikati ya Tanzania walionekana wana hoja nzito.Suala hilo likafikia hatua ya kukatiwa shauri na wabunge wakawa wanalikwepa baada ya kuona litagharimu fedha nyingi, hivyo ikabidi pendekezo hilo liahirishwe na mwaka uliofuata pia likahairishwa.

Hata ilipofika wakati wa kujadiliwa na baraza la mawaziri ilionekana gharama zake ni kubwa na kuonesha hicho ndio kitu kinachoshindikana kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi.Hata hivyo, kumbukumbu zinaonesha kwamba Februari mwaka 1966, Mbunge wa Musoma wa wakati huo, Hayati Joseph Nyerere (kaka yake Mwalimu Nyerere) aliwasilisha bungeni muswada binafsi, akipendekeza Dodoma iwe makao makuu ya nchi.

Katika mapendekezo yake alisema Dar es Salaam inahudumia sehemu ndogo tu ya nchi na kwamba endapo makao makuu ya serikali yatakuwa Dodoma hapana shaka, jambo hilo litasogeza nchi karibu sana na watawala.

Pia alisema mji wa Dodoma tangu zamani umekwishakuwa na ule ubora wa kuwepo katika njia ya reli itokayo Mashariki mpaka Magharibi Makao Makuu ya Tanu Taifa yakiwa yameambatanishwa na hoja zote zilizotolewa miaka ya nyuma.

Maazimio ya Mwanza yakazungumzwa katika mkutano wa Taifa wa Tanu na majadiliano hayo yalifikia kilele chake kwa kuhamia Dodoma ni sababu za kiuchumi kwa wakati huo.

Anataja sababu hizo kuwa ni kuyumba kwa uchumi duniani kulikoiathiri pia Tanzania, kupanda kwa bei ya mafuta na uchumi wa Tanzania kuyumba kutokana na vita ya Kagera.



Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan umefanya juhudi kubwa katika kuendeleza mpango wa kuhamisha makao makuu ya serikali Dodoma, ambao takribani wizara nyingi kama si zote na taasisi muhimu za serikali zimehamia ni jambo linaloubeba kuwa makao makuu ya nchi.

Akazidi kupiga debe akisema mji huo upo katika njia panda inayoziunganisha barabara kuu nne.Alisema kuhamisha makao makuu Dodoma kungeimarisha mawasiliano ya dhati na kungeharakisha shughuli ndogo ndogo na kwamba yeye kama mbunge wa Musoma, ni rahisi kufika Dodoma kuliko Dar.

Hoja alizotoa ziliungwa mkono na watu wengi wakiwemo wabunge wenzake lakini pingamizi zikatolewa kwamba ni gharama nyingi kutekeleza hilo.

Hata hiyo, kwa upande wa gharama, mbunge huyo alitoa shauri la kuhamishwa Idara za Serikali kidogo kidogo na si zote kwa pamoja.

Licha ya hayo bado suala la fedha bado lilikuwa na uzito mkubwa kutokana na rai aliyoitoa Makamu wa Pili wa Rais wakati huo, Rashidi Kawawa na likatolewa shauri pendekezo hilo lifikiriwe kwa umakini zaidi.

Ilipofika mwaka 1972 shauri hilo likachukuliwa na Kamati Kuu ya chama cha Tanu ya Mkoa wa Mwanza na kuwapa wanachama wake kuijadili. Tanu (Tanganyika African National Union) ndicho kilichokuwa chama tawala wakati huo kabla ya kuungana na Afro Shirazi Party (ASP) na kuzaa CCM.

Wanachama wa Tanu Mwanza waliona ilikuwa busara kuhamishia makao makuu ya chama chao na ya serikali Dodoma ambako ni katikati mwa nchi wakiamini hilo litaharakisha maendeleo.

Maazimio hayo yalipelekwa kupigiwa kura katika vikao vya Tanu mikoani na kwenye matawi.

Matokeo ya kura hiyo yalionesha kwamba mikoa 18 iliunga mkono pendekezo la makao makuu ya nchi kuhamishiwa Dodoma na mikoa mitatu ilipinga shauri hilo. Tanzania ilikuwa na mikoa 21 wakati huo. Kwa sasa Tanzania ina mikoa 31.

Halikadhalika matawi ya Tanu yaliyokubali wazo hilo yalikuwa 1,859 na yaliyopinga yalikuwa 842. Kutokana na kura hizo, Dodoma ikakatiwa shauri kuwa makao makuu ya Tanzania.

Rais wa kwanza wa Tanzania na Mwenyekiti wa Tanu, Mwalimu Julius Nyerere akapigia mbiu matokeo ya kura hiyo maoni ya kutaka Dodoma iwe makao makuu ya nchi Oktoba mosi, 1973 katika mkutano wa 16 wa Tanu uliokuwa ukifanyika kila baada ya miaka miwili. Uamuzi huo ulipokelewa kwa shangwe.

Mwalimu Nyerere alisema makao makuu ya kitaifa ni kitu cha kudumu na gharama za kujenga makao makuu ya kitaifa ni kitu cha muda mfupi.

Rais Nyerere pia akatangaza kuwa serikali inachukua hatua za haraka kutekeleza uamuzi huo na mnano Oktoba 6, vikaundwa vikosi viwili kutekeleza azimio hilo navyo ni Wizara ya Uimarishaji Makao Makuu na Mamlaka ya Uimarishaji Makao Makuu.

Kazi ya ujenzi wa makao makuu ikawa imeanza lakini kwa mujibu wa aliyekuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA), Mzee Pius Msekwa, anasema kilichomkwamisha Mwalimu

Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani, Rais John Magufuli na aliyekuwa makamu wake, Samia Suluhu Hassab walimeamua kutekeleza wazo hilo la kuhamia Dodoma kama alivyotaka Mwalimu Nyerere kwa vitendo bila kuangalia nyuma.

Mambo mengi yalishafanyika katika kipindi kifupi katika kutekeleza dhamira hiyo wakati wa utawala wa awamu ya tano. Baadhi ya mambo hayo yalikuwa ni kupitisha sheria rasmi inayoitambua Dodoma kama makao makuu ya serikali, kuifanya Dodoma kuwa jiji na wizara kadhaa pamoja na viongozi wakuu wa serikali kama Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kuhamia Dodoma.

Mzee Msekwa aliwahi kuulizwa kama suala la kiuchumi haliwezi kukwamishwa tena nia njema ya kuhamia Dodoma kama ilivyotokea enzi za Mwalimu Nyerere na kwamba hata kabla Mwalimu hajatangaza nia hiyo rasmi, watu wengi wakiwemo wabunge walihofu gharama za kuhamia Dodoma.

Akijibu swali hilo, Msekwa anasema wakati ule kwa sera zilizokuwepo, kila kitu kilikuwa kinaitegemea serikali, lakini kwa sasa hatua ya kuhamia Dodoma inafanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Alitolea mfano wa mfanyabiashara Hayati Mustafa Sabodo aliyeahidi kutumia mabilioni ya pesa kuwekeza Dodoma ili kuunga mkono mpango wa kuhamia Dodoma.

Katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia ... Dodoma.

Rais Samia pia amendeleza miundombinu ya kisasa kama vile barabara, maji, na umeme ili kuhakikisha kuwa Dodoma inakua kwa kasi na inaweza kuwa kituo cha serikali na biashara. Hii ni pamoja na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dodoma na miradi ya barabara kuu.

Rais Samia ameimarisha huduma za kijamii kwsa kuweka mkazo katika kuboresha huduma za afya, elimu, na usafiri katika mji wa Dodoma, ikiwa ni sehemu ya kuifanya Dodoma iwe mji unaofaa kwa wafanyakazi wa serikali na wakazi wake.


Uhamisho wa watumishi wa umma: Kwa kupitia sera za serikali, amesimamia na kuendeleza uhamisho wa watumishi wa umma kwenda Dodoma. Mpango huu unalenga kuhakikisha kwamba wizara zote na taasisi kuu za serikali zinafanya kazi kutoka Dodoma.

Kukuza uchumi wa Dodoma: Rais Samia ameweka kipaumbele katika kukuza uchumi wa mji wa Dodoma kwa kuvutia uwekezaji na biashara. Hii ni juhudi za kuifanya Dodoma kuwa jiji la kibiashara na kuwa na mvuto wa kimataifa.

Kushirikiana na sekta binafsi: Amehimiza ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika ujenzi wa nyumba, ofisi, na miundombinu mingine ambayo itasaidia kufanya mji wa Dodoma uwe kivutio cha watu wa kada mbalimbali.

Kupitia juhudi hizi, Rais Samia anaendeleza dhamira ya kuifanya Dodoma kuwa makao makuu rasmi ya serikali na kuwa jiji linaloendana na hadhi ya makao makuu ya taifa.





# Rais Dk. Samia kama Mwalimu Nyerere elimu ya kujitegemea

**Na Mwandishi Wetu**

"NI wazi wakati umefika sasa tufikirie sana juu ya swali hili: 'Mpango wa Elimu Tanzania umewekwa kwa sababu gani, shabaha yake ni nini?"

Mwalimu Julius Nyerere alijiuliza swali hilo mwaka 1967 wakati akiwa katika mchakato wa kutangaza Azimio la Arusha, kisha akalipatia jibu kwa kuja na Elimu ya Kujitegemea.

Muda wote, shabaha kuu ya elimu imekuwa ni kurithisha maarifa na mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine na kuwaandaa vijana wawe tayari kuchukua nafasi zao katika kulitumikia na kuliendeleza taifa.

Mwalimu alifanya mambo mengi katika elimu ikiwemo kuja na Azimio la Musoma la mwaka 1974 ambalo lililenga kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule anakwenda shule, kutoa elimu bila malipo na mengine lukuki.

Hata hivyo, makala haya yataangalia zaidi eneo la elimu ya kujitegemea iliyokwenda sambamba na falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea na namna serikali ya awamu ya sita inavyokuja na falsafa inayoendana na ya Mwalimu Nyerere katika eneo la kujitegemea. Tukumbuke, Mwalimu alipata kusema unaweza ukaachana na ujamaa lakini huwezi kuachana na dhana ya kujitegemea.

Baada ya uhuru, Mwalimu alijua kwamba elimu ambayo Tanzania ilirithi kutoka kwenye serikali ya kikoloni ilikuwa ina upungufu kadhaa na isingesaidia kuwafanya wananchi kufanya mabadiliko katika maisha yao na taifa lao. Ni katika mkutadha huo, Mwalimu alipata kusema kwamba 'ukitaka kumsaidia mtoto wa maskini, mpe elimu.'

Baadhi ya upungufu wa elimu hiyo ni kujenga fikra za kuajiriwa katika sekta ya umma, huku ikimfanya mhitimu ajione yeye ni bora au bwana mkubwa kulinganisha na Watanzania wenzake ambao hawakubahatika kupata elimu kama yake.

Katika hotuba yake aliyoitoa mwaka 1967, Mwalimu Nyerere alisema ni muhimu Tanzania sasa itazame kama muundo na elimu yenyewe inayopatikana inafaa kwa kazi inayotakiwa kufanya.

## MWALIMU ALITAKA WATOTO WAJIFUNZA UZALISHAJI

Akizungumzia falsafa ya Mwalimu Nyerere juu ya elimu ya kujitegemea, mchambuzi Alexander Mhando katika andiko lake moja anasema kwamba Mwalimu alilenga kuwajenga vijana kujifunza zaidi kazi za uzalishaji mali wakiwa shuleni, na kuziwezesha shule zijitegemee kutokana na uzalishaji huo.

Mbali na kujitegemea, kazi hizo zililenga kuwawezesha wanafunzi kujengwa kwa namna ambayo inawapevusha fikra zao, na hivyo kuleta mtazamo chanya wa mabadiliko ya kweli katika jamii kufuatana na ujuzi wanaoupata.

Kwamba mbali na wanafunzi kupewa elimu ya darasani, vilevile wawe wanapewa elimu ya stadi za maisha.

Mhando katika andiko lake linalopatikana kwenye mtandao wa kompyuta anasema: "Dhana hii ya Mwalimu Nyerere aliyoiasisi juu ya elimu ya kujitegemea iliondoa upungufu mwingi uliokuwepo kwenye elimu ya mkoloni ambayo haikuwaandaa watu kujitegemea na kufanana na maisha ya kitanzania pamoja na kuwafanya wanafunzi watambue wajibu wao kwa jamii baada ya kumaliza shule na vyuo vikuu."

Mapinduzi haya ya elimu yalilenga kumfanya mtoto anayemaliza elimu ya msingi au sekondari awe tayari na stadi fulani za maisha na fikra za kujitegemea huku akiwa na uwezo wa kuzalisha mali.

Kwa mfano, Mwalimu katika hotuba aliyotangaza elimu ya kujitegemea, alisema: "Kama watoto wa shule za msingi wanafanya kazi katika shamba la ushirika la kijiji, tuseme wamegawiwa kipande chao maalumu kukiangalia, basi watajifunza maarifa mapya ya kilimo na kujivunia mafanikio ya shule yao. La kama hakuna shamba la ushirika kijijini basi shule inaweza kuanzisha shamba lake yenyewe kwa kuwaomba wale walio wakubwa zaidi wafyeke misitu wakati watoto wengine wanapofanya kazi nyingine za jumuiya."

## ELIMU YA AMALI

Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa pia ikijitahidi kuvaa viatu vya Mwalimu Nyerere katika kuboresha elimu nchini kwa kuakisi mahitaji ya sasa ya elimu nchini.

Kwa mujibu wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, elimu ya msingi sasa ni miaka sita na sekondari miaka minne. Kwamba hatua hii inakwenda sambamba na kuwapa fursa wanafunzi kuchagua aina ya masomo wanayoyapenda, yakiwemo ya amali (ufundim, stadi na vitendo) na kusaidia waweze kujiajiri wamalizapo masomo.

Waziri anasema wakati somo la Kiingereza litakaziniwa kufundishwa kuanzia darasa la kwanza, baada ya darasa la sita kutakuwa na mkondo wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi utakaojulikana kama elimu ya amali na elimu ya jumla.

Mbali na Somo la Kiingereza, masomo mengine mapya yatakayofundishwa ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) na stadi za maisha.

Anasema kila mkondo kutakuwa na michepuo yake, ili kuwapa nafasi wanafunzi kuchagua masomo wanayoyataka kwa ajili ya kuendeleza ujuzi na nadharia zaidi ili wakimaliza shule waweze kujiajiri wenyewe.

Sera mpya ya elimu pia inalenga kuweka mazingira wezeshi ya kuongeza ushiriki wa wasichana katika elimu ya amali na elimu ya juu hususani katika fani za sayansi, hisabati na tekonolojia.

Waziri Mkenda anasema rasimu ya mapitio ya mitaala ambayo imekamilika na sasa inaendelea kujadiliwa imefanyiwa kazi kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo maaskofu, mashehe, walimu, wamiliki wa shule binafsi pamoja na wataalamu kutoka nje ya nchi ili kupata uzoefu kutoka katika nchi zilizoleta mageuzi ya elimu.

Katika muktadha huo, wizara pia imeboresha mahusiano kati ya wadau na wadau kama sekta ya viwanda na waajiri ili kuweza kupata kitu ambacho ni kizuri zaidi.

## ELIMU BILA MALIPO

Wakati serikali ya awamu ya tano ilirudisha elimu bila malipo hadi kidato cha nne, serikali ya awamu ya sita chini ya Dk. Samia Suluhu Hassan imeongeza kutoa elimu bila malipo hadi kidato cha sita na kuongeza maradufu kiwango cha mikopo kwa elimu ya juu.

Hatua hii ina lengo na shabaha ya kuwasaidia watoto wote wa Tanzania kupata elimu bila kujali tofauti zao za kiuchumi katika familia zao, dhana ambayo Mwalimu aliisimamia sana.

Kabla ya elimu bila malipo, mtoto wa maskini alikuwa na nafasi finyu ya kusoma hadi elimu ya juu ikilinganishwa na mtoto anayetoka familia yenye uwezo kiuchumi.

Ni kwa msingi huo, wakati huu ambao serikali inafanya maboresho katika sera ya elimu na mitaala, watoto wa Tanzania bila kujali vipato vyao wazazi wao, watanufaika kwa ajili ya wao wenyewe na taifa kwa ujumla.

Wakati serikali ikiboresha elimu ya ufundi hususani katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri ama kuajiriwa, mtazamo huo pia umepelekwa kwenye shule za msingi na sekondari katika kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia.

Hakika ni jambo la kushukuru kuona serikali ya awamu ya sita imejiuliza kama alivyojiuliza Mwalimu mwaka 1967 kwamba 'mpango wa elimu Tanzania umewekwa kwa sababu gani, shabaha yake ni nini katika zama tulizo nazo?' Baada ya kujiuliza inakuja na mabadiliko chanya kwenye sera na mitaala ya elimu ili kuendana na wakati wa sasa.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Ubia wa serikali na sekta binafsi muhimu kuharakisha maendeleo



Tuko katika siku za kumbukumbu ya miaka 25 toka taifa liondokewe na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Enzi za uhai wake, Mwalimu aliwahi kusisitiza kuwa juhudi zinazofanywa na serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo ni lazima ziguse maisha ya watu.

Akasisitiza kuwa maendeleo yasiyogusa maisha ya watu hayana maana, ni lazima maendeleo yaguse maisha ya wananachi, kwani hayo ndiyo maendeleo yenye maana, maendeleo ya watu.

Maendeleo ya watu yanaambatana na utekelezaji na uboreshaji wa miradi ya maendeleo. Miradi ya maendeleo kama vile shule, vyuo, hospitali, maji, umeme, barabara, ofisi, masoko, mabwawa na mingine kadha wa kadha inapotekelezwa kikamilifu, inagusa maisha ya watu hasa katika kuboresha maisha ya wananchi ambapo uwepo wa miradi hiyo huleta manufaa katika maisha.

Kimsingi, serikali inawajibika moja kwa moja katika kuhakikisha wananchi wanapata maendeleo kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu, serikali inayo wajibu wa kuleta ustawi katika maisha ya wanachi wake.

Njia mojawapo ya kuleta ustawi katika maisha ya wananchi ni kuibua miradi ya kimkakati na miradi mingine ili kwa pamoja wananchi wanufaike na hivyo ustawi wa maisha ya wananchi uwe ni halisi.

Miongoni mwa jambo ambalo limepewa msukumo mkubwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi (Public and Private Partnership – PPP). Ndiyo maana Januari 5, 2022, Rais Dk. Samia alimteua David Kafulila kuwa Kamishna wa Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, ili kuwe na msukumo wa kipekee katika ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika kuchagiza miradi ya maendeleo kwa ustawi wa wananchi.

Ni katika ushirikiano huu ambao kwa kiasi kikubwa serikali imepunguziwa mzigo katika kuboresha maisha ya wananchi kwani sekta binafsi inashirikishwa kikamilifu katika ujenzi wa nchi.

Ni ukweli ulio dhahiri kuwa ujenzi wa nchi unahitaji juhudi za pamoja. Ni bahati mbaya wakati mwingine baadhi ya wananchi wamekuwa na dhana potofu kwa kudhani serikali peke yake ndiyo yenye wajibu wa kufanya kila kitu bila kujua kuwa hata mtu binafsi, kampuni, taasisi zisizo za kiserikali, asasi za kiraia nao ni sehemu katika ujenzi wa nchi yaani wanapaswa kushirikiana na serikali katika kutatua kero za wananchi kwa kuibua miradi ya maendeleo yenye tija katika maisha ya wananchi.

Ni muhimu kuhakikisha kuwa miradi ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi inaibuliwa ili kutatua kero za wananchi badala ya kutegemea na kusubiria fedha kutoka serikalini kutatua kero za wananchi.

Sekta binafsi ni mdau muhimu wa maendeleo, na pale kunapokuwa na sekta binafsi imara, kasi ya maendeleo nayo inakuwa kubwa na hivyo maisha ya wananchi yanakuwa bora zaidi. Kunahitajika uzoefu, utaalamu na raslimali fedha za kutosha katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo basi, serikali peke yake inalemewa, na hivyo, ubia kati ya serikali na sekta binafsi ni muhimu sana ili kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa mfano, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kushirikiana na Kituo cha Ubia wa Sekta za Umma na Binafsi (PPP) wameshirikiana ili kufanikisha azma ya kujenga mabweni ya wananchi kwa ubia utakaogharimu shilingi bilioni 20.7.

Kwa mujibu wa Mkuu wa chuo cha CBE, Prof. Edda Lwoga, ubia huu unatokana na changamoto ya mabweni katika chuo cha CBE ambapo katika kampasi yake kuu jijini Dar es Salaam, chuo kina wanafunzi 12,000 lakini mabweni yaliyopo ni mawili tu yenye uwezo wa kuchukua vitanda 160 pekee vya wanafunzi wa kike na kiume. Vitanda hivi 160 ni sawa na aslimia 1.34 huku kukiwa na upungufu wa vitanda kwa asilimia 98.6.

"Mradi huo utafanywa kwa ubia kati ya CBE na mwekezaji lakini pia naomba nitumie nafasi kuwafahamisha wadau, wawekezaji wa ndani na nje kuhusu fursa hii muhimu ya uwekezaji ili waweze kushiriki kwenye mkutano maalumu utakaokutanisha wadau mbalimbali katika kuupelekea mradi huu sokoni na kupeana uwelewa zaidi na mkutano huo utafanyika tarehe 20 siku ya ijumaa," alisema Prof. Lwoga.

Ubia kati ya serikali na sekta binafsi ni muhimu kutokana na uwepo wa changamoto nyingi zinazowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Nguvu ya pamoja baina ya sekta hizi mbili inachagiza utatuzi wa kero za wananchi kwa kuzingatia kuwa umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Uwepo wa uhitaji mkubwa wa mabweni katika chuo cha CBE utapungua kwa kutoka asilimia 1.34 iliyopo sasa hadi asilimia 30 pindi mradi huu wa ujenzi wa mabweni utakapokamilika.

"Hali iliyopo imesababisha uhitaji mkubwa wa malazi ya wanafunzi kwa asilimia 98.6 hivyo wengi wanalazimika kutafuta malazi nje ya chuo kwa gharama kubwa, jambo linalosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu gharama hizo. Njia ya PPP ni bora na ya haraka kufanikisha mradi huu, ambayo itawanufaisha wanafunzi na taasisi. CBE imejikita katika kutoa mazingira bora ya kujifunzia na uboreshaji malazi ya wanafunzi ni kipaumbele muhimu kwetu nawashukuru washirika wa sekta binafsi, serikali na wadau wote kwa mchango wao katika kufanikisha mradi huu muhimu," anasema Prof. Lwoga.

Septemba 20, 2024, Kamishna wa PPP, David Kafulika alipongeza ubunifu uliofanywa na CBE katika kutatua changamoto ya mabweni, na hivyo kutoa wito kwa vyuo vingine kuihusisha sekta binafsi katika ujenzi wa mabweni na miradi mingine ya maendeleo.

"Kila mradi ambao sekta binafsi inaweza kuutekeleza kwa teknolojia ya hali ya juu kuliko serikali basi apewe autekeleze ili tujenge uchumi wa kisasa ambao sekta binafsi ndiyo ina nafasi kubwa ya kutengeneza ajira nyingi. Utaratibu wa ubia unaleta unafuu kwa serikali kwa sababu miradi inajengwa bila kutegemea fedha zake lakini utaratibu huu wa ubia unafanya serikali ivute teknolojia ya kujenga baadhi ya miradi, teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa inapatikana sekta binafsi," amesema Kafulila.

Sekta binafsi ina nguvu ya raslimali fedha, ujuzi, uzoefu na teknolojia katika kumudu majukumu ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kwa hiyo, ni muhimu kwa viongozi serikalini kuishirikisha ipasavyo sekta binafsi katika miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuongeza kasi ya utatuzi wa kero za wananchi.

Sanjari na hilo, ni muhimu kuzingatia kuwa ubia kati ya serikali na sekta binafsi si ubinafsishaji. Ubia ni kuunganisha nguvu ya pamoja, miradi ya ubia inabaki kuwa mali ya serikali, huku sekta binafsi ikiwa mshirika muhimu, na baada ya sekta binafsi kurejesha gharama zake za uwekezaji kwa mujibu wa mikataba, miradi hiyo huwa mali ya serikali kwa asilimia 100.


Si hili la mabweni tu lililofanywa na uongozi wa chuo cha CBE, yapo mengi katika sekta nyingine kama vile maji, afya, umeme, mifugo, uchumi wa buluu, barabara, vivuko, kilimo, uvuvi, ambapo sekta binafsi inaweza kushirikishwa kikamilifu na kuifanya nchi kukimbia katika kujiletea maendeleo badala ya kutembea. Ni vyema sekta binafsi ikapewa ushirikiano badala ya kuwekewa vigingi kwani ni wadau muhimu wa maendeleo. Naamini miradi ya ubia ni muhimu sana hasa katika kuongeza kasi ya utatuzi wa kero za wananchi.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*

Paul Mng'ong'o
KLINIKI YA FIKRA
Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

WEWORK CONSULT

# Fanya haya kupata maendeleo binafsi



Dhana ya Maendeleo Binafsi (Personal Development) inahusisha mchakato wa wewe mtu binafsi kuboresha maisha yako kwa njia mbalimbali ili kufikia uwezo wako kamili, iwe kwa upande wa kitaaluma, kibinafsi, au kihisia.

Dhana hii inalenga kuongeza maarifa, ustadi, uwezo, na ufahamu wako wa mambo ili uweze kuishi maisha yenye maana zaidi na yenye mafanikio. Kama unataka kuendelea ni muhimu sana uzingatie mambo yafuatayo kwenye maisha yako. Bila mambo haya yanayoelezewa hapa chini, usifikirie kabisa dhana ya maendeleo yako binafsi. Vipengele hivyo vya ukuaji binafsi ni kama ifuatavyo:-

1. Kujiwekea malengo – Mpango wa maendeleo yako unaanza na hatua ya kubaini unachotaka kufanikisha katika maeneo tofauti ya maisha yako, kama kazi, mahusiano, afya au kipato. Watu wengi wanafanya kazi, wanasoma au kutekeleza majukumu bila kujua wanatamani kufikia hatua gani mwisho. Bila kuona hatma na unacholenga, huwezi kuzalisha nguvu (energy) kukufikisha unapopahitaji.
2. Kujitambua – Hatua ya pili kuelekea maendeleo yako ni kuelewa nguvu zako, udhaifu wako, thamani zako, na nini kinakupa motisha. Kujitambua kinakupa uelewa wa maeneo ya kuwekeza nguvu kubwa na maeneo ya kuyapunguza ndani yako. Hivyo unaelekeza nguvu nyingi kwenye eneo ambalo una nguvu nalo zaidi. Hii inakupa msingi wa kufanya maamuzi bora.
3. Kujifunza – Hatua ya tatu ya maendeleo yako ni kuweka jitihada za kujifunza ujuzi mpya au maarifa kwa njia ya masomo rasmi au isiyo rasmi ili kujiendeleza. Ni muhimu kujifunza kila kitu na kisha kujifunza kwa undani kwenye mambo ambayo yanaendana na nguvu zako na malengo yako ya msingi.
4. Kujiendeleza kihisia (Emotional Development) – Hatua nyingine muhimu na ambayo watu wengi hawafanyi ni kuweka juhudi katika kuboresha jinsi unavyoshughulika na hisia zako, yaani kuwa na udhibiti bora wa hisia, na kuelewa hisia za wengine (empathy). Ni muhimu sana kushughulika na hisia zako.
5. Kujenga nidhamu – Hatua nyingine muhimu sana kwenye hatua za maendeleo yako ni kuweka na kufuata ratiba au mazoea ambayo yatakusaidia kuboresha utendaji wako wa kila siku. Acha kabisa kutenda kwa mazoea. Jenga ratiba ya mambo yako ya msingi, yape nafasi na jenga nidhamu kubwa ya kutekeleza mambo yako kwa ratiba.
6. Afya ya mwili na akili – Pamoja na hatua hizo, ni muhimu sana kuipa kipaumbele afya yako kwa njia ya mazoezi, lishe bora, na kutunza afya ya akili kwa njia ya mindfulness au kupunguza msongo wa mawazo. Hii itakupa uwezo wa kusimamia malengo yako kikamilifu sababu afya yako ya mwili na akili vinakuwa vizuri na utulivu.

Pamoja na hayo, unapozingatia suala zima la maendeleo binafsi kwa ajili yako, ni muhimu kutambua mambo yafuatayo:-

- Ni mchakato endelevu: Maendeleo binafsi si jambo la mara moja bali ni mchakato unaoendelea. Hakuna maendeleo yaliyosimama, ni ama unaendelea au unarudi nyuma. Siku utakayoacha mchakato wa kutekeleza malengo yako halisi ya ukuaji, ndiyo siku utakayoanza kushuka kimaendeleo. Kutokana na ukweli huu, ni muhimu kujitathmini mara kwa mara na kufanya marekebisho inapobidi.
- Ni muhimu kuweka malengo yanayopimika: Ili maendeleo binafsi yawe na maana, malengo yanayowekwa yanapaswa kuwa mahususi, yanayopimika, yanayoweza kufikiwa, yanayohusiana na maisha yako, na yenye kipimo cha muda (SMART goals).
- Ni muhimu kuzingatia uboreshaji wa ustadi: Kujitolea muda kujifunza au kuboresha ustadi na tabia zinazohitajika kwa ajili ya kufanikisha malengo hayo ni suala la msingi mno. Mambo yanabadilika kila siku ni muhimu kujifunza mambo mapya na kufanya maboresho kwenye ustadi wako
- Ni muhimu kuzingatia msaada wa nje: Mara nyingi, watu wanafanikiwa zaidi wanapopata msaada kutoka kwa wengine kama vile walimu, wafanyakazi wenza, au hata makocha wa maisha (life coaches). Kuna watu wengi wanaamini kwenye kazi zao wenyewe na mipango pekee. Hawa wanachelewa sana kuendelea. Siku zote inua macho, angalia msaada, angalia mbinu mpya, angalia washauri wazuri angalia watu wanaoweza kukuonesha changamoto kwako na kukushauri, tafuta mentors, tafuta vipaji vya kukusaidia, nk. Utaendelea vizuri na kwa haraka.

Dhana hii inalenga kubadilisha maisha ya mtu ili aweze kuwa toleo bora zaidi la nafsi yake, kwa kuleta mabadiliko chanya kwenye nyanja mbalimbali za maisha.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa taasisi, kikundi, kanisa, umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

Wework Consult
Your Partner in Growth.

# Utata wa kifo cha John F Kennedy wa Marekani - 4

**Tunaendelea na simulizi za utata wa kifo Rais wa 35 wa Marekani John Fitzgerald Kennedy aliyeingia ofisini Januari 20, 1961 hadi alipouawa Novemba 22 mwaka 1963. Ikiwa ni miaka 61 imepita tangu kifo hicho, tumeangalia safari yake ya kutembelea Jimbo la Texas akiwa na malengo kadhaa, kubwa likiwa ni kujiimarisha kisiasa katika jimbo hilo baada ya kutofanya vizuri sana katika uchaguzi uliokuwa umemwingiza madarakani. tulianza kuangalia namna safari yake ilivyotangazwa, maofisa usalama walivyokagua maeneo ya kupita, safari ilipoanza kwa njia ya gari kutoka Kiwanja cha Ndege cha Love Field kuelekea Dallas Trade Mart, katikati mwa jiji la Dallas, Jimbi la Texas pamoja na mpangilio wa magari ulivyokuwa. Mwandishi Wetu, HAMID YASSIN kuangalia kilichotokea wakati gari lake limefika eneo ambalo alipigwa risasi.**

Majira ya saa 6 na dakika 29 msafara wa Rais uliingia katika eneo kubwa (mtaa) ujulikanao kama 'Dealey Plaza' ambao zamani ulikuwa na bustani na maeneo ya watu kupumzika. Mbele ya macho yao lilikuwa linaonekana "jengo lililobeba kifo" cha Rais Kennedy, Jengo la 'Texas School Books Depository'. Kwa kuzingatia kuwa Kennedy alipata kura kiduchu eneo hili la Dallas wakati wa uchaguzi mkuu, hivyo mkewe Jackie akamgeukia na kumtania. "Kwa hizi shamra shamra, huwezi kusema eti wananchi wa Dallas wanakuchukia…," Jackie akaongea huku anatabasamu kumuangalia mumewe. "Hakika! Siwezi kusema wananichukia!" Kennedy akamjibu kwa kifupi mkewe huku anatabasamu na kuwapungia mikono wananchi. Na hii ndio ilikuwa kauli ya mwisho ya Rais JF Kennedy… tayari ilikuwa ni saa 6 na 30. Na mbele yake alikuwa amebakiza chini ya sekunde 15 za uhai wake.

Risasi ya pili kumpata rais (ambayo ilikuwa ni risasi ya tatu kupigwa) ilimpata kichwani upande wa juu kulia. Risasi hii ilifumua kabisa eneo hilo la kichwa na kusababisha sehemu ya ubongo wa mbele kumwagika.

Damu nyingine ikaruka nyuma ya gari kwenye 'trunk' na nyingine kutua mpaka kwenye mkono wa kushoto wa afisa wa 'Secret Services' aliyekuwa anaendesha gari ya wanausalama waliokuwa gari ya nyuma ya Rais.

Ndani ya sekunde mbili baada ya mumewe kufumuliwa na risasi kichwani, First Lady Jacqueline Kennedy akaruka kutoka kwenye siti yake na kuanza kuparamia nyuma ya gari kwenye 'trunk'.

Tofauti na wengi wanavyodhani kwamba alikuwa anajaribu kukimbia kuokoa maisha yake, ila ukweli ni kwamba alikuwa anaokota kipande cha mfupa wa fuvu la kichwa kilichodondoka kwenye nyuma ya gari kwenye 'trunk' baada ya mumewe kufumuliwa kichwa na risasi.

Baada ya kukichukua haraka haraka akarejea kwenye siti yake.

Sekunde hii hii ambayo First Lady alikuwa anaparamia gari kwenye 'trunk', katika gari ya nyuma, 'Special Agent', Clint Hill ambaye alikuwa ananing'inia kwenye mlango wa mbele kushoto akaruka na kuanza kuikimbilia gari iliyombeba rais na First Lady.

Dereva wa gari la rais alikuwa ameongeza mwendo baada ya mushkeli kutokea na dhahiri kuonekana kwamba rais yuko hatarini.

Hivyo basi ilimbidi Clint Hill kujaribu kuparamia gari mara kadhaa mpaka alipofanikiwa kuidandia gari na mara moja kuwafunika rais na First Lady akiwakinga kwa kutukia mwili wake kama ngao.

Baada ya Agent Clint Hill kuwakinga Rais na mkewe dhidi ya shambulio lingine lolote la risasi kuwafikia, gari ya rais liliendeshwa kwa kasi kubwa likifuatiwa na pikipiki za pembeni na ile gari ya nyuma ya maafisa usalama.

Wakati haya yote yanatokea zilikuwa zimebaki takribani dakika tano pekee kufika walikokuwa wanaelekea, Trade Mart.

Kwa hiyo baada ya gari iliyombeba Rais kuanza kuendeshwa kwa kasi, takribani saa 6 na dakika 35 walipita eneo la Trade Mart na kuelekea moja kwa moja hospitali ya Parkland Memorial Hospital ambako waliwasili majira ya saa 6 na dakika 38 na kupokelewa kisha Rais Kennedy alipelekwa moja kwa moja chumba cha dharura.

Licha ya watu wa usalama kujitahidi sana kuratibu taarifa za kilichotokea zisivuje kabla ya taarifa rasmi ya serikali, lakini majira ya saa 6 na dakika 40 kituo cha televisheni cha CBS kikakatisha Igizo lililokuwa linaonyeshwa kwenye televisheni yao na kutoa "Breaking News" kuwa msafara wa Rais umeshambuliwa huko Dallas.

Baadaye kama muda wa saa 6 na dakika 45, Dan Rather mwandishi wa habari wa kituo cha CBS alifanya mawasiliano kwa siri sana na daktari anayemfahamu hapo hospitalini na kuvujishiwa taarifa kuwa kuna uwezekano mkubwa Rais Kennedy hayuko hai.

Ifahamike kwamba maafisa wa 'Secret Services' waliwaleta hapa viongozi wengine wote wakuu waliopo kwenye msafara, yaani First Lady Jacqueline Kennedy, Makamu wa Rais Johnson, Mkewe Lady Bird na Gavana Connally ambaye alikuwa chumba cha wagonjwa mahututi.

Ilipofika saa 7 kamili madaktari wakatoa taarifa yao kwa viongozi wa serikali na wanausalama waliokuwepo hapo kwamba, licha ya kutumia ujuzi wao wote na maarifa yao yote, wameshindwa kuokoa maisha ya Rais JF Kennedy, kwamba Rais Kennedy amefariki dunia!!

Huko mtaani habari zilikuwa zinaenea kwa kasi kama moto wa kifuu, kuwa Rais Kennedy amefariki, hivyo kwa busara watu wa usalama wakashauri kuwa itolewe taarifa rasmi kuhusu kifo cha Rais Kennedy ili kuepusha mkanganyiko na taharuki iliyopo mtaani.

Makamu wa Rais Johnson akakubali hilo lakini akaamuru taarifa hiyo itolewe kwa umma mara baada ya yeye kuondoka hapo hospitali kwa sababu ya usalama wake, kwamba hataki yeyote ajue kuwa yuko hapo hospitali kwa kuwa kwa vile Rais ameuwawa tayari yawezekana yeye kama Makamu wa Rais akawa ni "next target"!

*Itaendelea*



**Dan Rather mwandishi wa habari wa kituo cha CBS alifanya mawasiliano kwa siri sana na daktari anayemfahamu hapo hospitalini na kuvujishiwa taarifa kuwa kuna uwezekano mkubwa Rais Kennedy hayuko hai.**



# Naibu Rais akanusha tuhuma za ufisadi




**NAIROBI, Kenya**

MAKAMU wa Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, juzi Jumatatu alikanusha madai ya ufisadi dhidi yake katika mkesha wa kura ya kutokuwa na imani naye ambayo inaashiria mgawanyiko mkubwa katika chama tawala.

Tuhuma hizo zinakasirisha na ni propaganda tupu, Gachagua alisema katika mkutano na waandishi wa habari, akizitaja kuwa jaribio la "kuniondoa madarakani kutokana na sababu nyingine za kisiasa."

Hakuna mashitaka rasmi yaliyofunguliwa na waendesha mashitaka na hakuna uchunguzi ulionzishwa na mahakama.

Lakini Gachagua alishindwa kuzuia mchakato wa kutokuwa na imani naye katika Bunge wiki iliyopita, licha ya kuwasilisha malalamiko mara kadhaa mahakamani akiomba mchakato huo usitishwe.

Makamu huyo wa Rais William Ruto, anatuhumiwa kwa ufisadi, kudhoofisha shughuli za serikali na kutumia siasa za kikabila zinazoleta mgawanyiko, kati ya mashitaka mengine.

Wabunge wa Kenya walianzisha mchakato wa kumfungulia mashitaka Oktoba mosi, mwaka huu huku wabunge 291 wakiunga mkono hoja hiyo, ikiwa zaidi ya kiwango cha wabunge 117 kinachohitajika. VOA.

> **Tuhuma hizo zinakasirisha na ni propaganda tupu, Gachagua alisema katika mkutano na waandishi wa habari, akizitaja kuwa jaribio la "kuniondoa madarakani kutokana na sababu nyingine za kisiasa."**

# 350 wapoteza maisha kwa kipindupindu

**ABUJA, Nigeria**

ZAIDI ya watu 350 wamefariki dunia kutokana na ugonjwa kipindupindu nchini Nigeria katika miezi tisa ya kwanza ya mwaka huu,

Hili ni ongezeko la asilimia 239 kutoka kipindi kama hicho mwaka jana, data kutoka Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Nigeria (NCDC) zilionyesha juzi Jumatatu.

Kipindupindu, ugonjwa unaotokana na maji machafu, si jambo lisilo la kawaida nchini Nigeria ambako mamlaka za afya zinasema kuna ukosefu wa maji ya kunywa katika maeneo ya vijijini na makazi duni ya mijini.

NCDC ilisema watu 359 walifariki dunia kati ya Januari na Septemba, mwaka huu ikilinganishwa na watu 106 katika kipindi kama hicho mwaka jana. VOA.




# Kais Saied ashinda tena urais Tunisia

**TUNIS, Tunisia**

RAIS wa Tunisia, Kais Saied, amechaguliwa kwa muhula mwingine kwa asilimia 90.69 ya kura, Tume ya Uchaguzi (ISIE) imesema.

Miaka mitatu baada ya Saied kujinyakulia mamlaka makubwa, makundi ya kutetea haki za binadamu yanahofia kuchaguliwa kwake kutaimarisha utawala wake katika taifa hilo ambalo demokrasia yake iliimarika kufuatia maandamano ya mwaka 2011.

Saied, mwenye umri wa miaka 66, alishinda kwa kishindo uchaguzi wa Jumapili kwa kura milioni 2.4, lakini asilimia 28.8 tu ndiyo walijitokeza kupiga kura kati ya watu milioni 10 wanaotimiza masharti ya kupiga kura.

Mpinzani wake anayefungwa jela Ayachi Zammel, alipata asilimia 7.3 na mgombea wa tatu Zouhair Maghzaoui alipata asilimia 1.9 ya kura, kiongozi wa ISIE Farouk Bouasker, alitangaza kwenye televisheni ya taifa.

VOA.



# Papa Francis kuteua makadinali wapya 21

**TEHRAN, Iran**

PAPA Francis atawateua makadinali wapya 21 kutoka duniani kote.

Hayo aliyasema siku ya hayo Jumapili, katika hatua ambayo haikutarajiwa kushawishi kundi hilo lenye nguvu la watu wa kanisa ambao siku moja watamchagua mrithi wake.

Hafla ya kuwaidhinisha wateule wapya, inayojulikana kama `consitory' itafanyika Disemba 8, mwaka huu Papa huyo mwenye umri wa miaka 87, alisema wakati wa ibada ya alasiri ya kila wiki na mahujaji na watalii katika eneo la Mtakatifu Petro.

Itakuwa hafla ya 10 kuitishwa na Papa tangu kuchaguliwa kwake miaka 11 iliyopita, kama Papa wa kwanza kutoka Amerika Kusini.

Makadinali hao wapya ni kutoka nchi tofauti ikiwemo Argentina, Brazil, Chile, Peru, Italy, Uingereza, Serbia, Japan, Indonesia, Canada, Ivory Coast na Algeria.

20 kati yao wana umri wa chini ya miaka 80 na watapiga kura katika kongamano kumchagua Papa mpya baada ya kifo cha Francis au kujiuzulu kwake.


Mmoja kati ya kundi hilo ana umri wa miaka 99, ni Askofu kutoka Italia. Askofu Mykola Bychok wa Kanisa Katoliki la Ukraine, ana umri wa miaka 44, atakuwa Kadinali wa kwanza mwenye umri mdogo.

VOA.

> **Makadinali hao wapya ni kutoka nchi tofauti ikiwemo Argentina, Brazil, Chile, Peru, Italy, Uingereza, Serbia, Japan, Indonesia, Canada, Ivory Coast na Algeria.**



# Utamaduni wetu baada ya Mwalimu Nyerere



Na Mwandishi Maalumu

NI miaka 25 sasa tangu kufariki kwa mwasisi wa taifa hili na Rais wa kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere Oktoba 14, 1999.

Mwalimu Julius Nyerere alikuwa ni kati ya viongozi wachache wa Afrika ambao wameacha athari chanya katika utamaduni wa nchi zao.

Nyerere alikuwa Mwalimu na hivyo ni sahihi pia kusema taaluma na silika ya ualimu iliathiri siasa na matendo yake pia kama kiongozi wa Tanganyika na baadaye Tanzania. Aliiona Tanzania kama darasa, na daima alikuwa anafundisha.

Yapo mengi kuhusu Mwalimu Nyerere lakini ninachotaka kuongelea hapa ni mchango wake katika uwanja wa sekta ya utamaduni.

Mwalimu Nyerere aliamini kuwa nchi isipoupa nafasi utamaduni wake isingeweza kufanikiwa katika baadhi ya mambo yakiwemo ya kujenga umoja, jamii inayojitambua, utaifa na hata uchumi, jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa Taifa.

Hata ripoti ya hivi karibuni ya Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), imeonesha jinsi bidhaa za kitamaduni zilivyo na mchango mkubwa katika kuchochea ukuaji wa uchumi, hususani katika kizazi hiki cha kidijiti.

Baada ya uhuru, Desemba 1961, Mwalimu aliunda Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana mwaka 1962, na alitamka wazi kuwa Utamaduni ni kiini na roho ya Taifa. Akasema nchi inayokosa utamaduni wake ni sawa na mkusanyiko wa watu usiokuwa na roho hivyo kukosa sifa ya kuitwa taifa kamili.

Tangu mwaka 1962, shughuli za sanaa na utamaduni zilipewa nafasi katika mfumo wa kiserikali.

Katika utawala wake uhusiano kati ya utamaduni na maendeleo ulitambuliwa, hasa miaka ya 70. Kwa mfano, iliyokuwa Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana (1979) iliwateua wataalamu wake waandike kitabu kiitwacho Utamaduni Chombo cha Maendeleo.

**Mwalimu Nyerere aliamini kuwa nchi isipoupa nafasi utamaduni wake isingeweza kufanikiwa katika baadhi ya mambo yakiwemo ya kujenga umoja, jamii inayojitambua, utaifa na hata uchumi, jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa Taifa.**

Katika dibaji ya kitabu hicho, aliyekuwa Waziri wa Wizara husika alitoa maelezo yaliyojaribu kuonesha uhusiano kati ya utamaduni, uhuru na maendeleo.

Sehemu ya Dibaji ilisema: "Kuna sababu nyingi za kuutambua Utamaduni kuwa ni chombo cha maendeleo. Moja ni kuwa vipengele na fani mbalimbali za Utamaduni ndizo zilizoko katika kiini cha umoja wa jamii.

Utamaduni ni sehemu ya siasa ya Taifa letu lenye msingi na shabaha ya umoja wa kweli. Uhuru wetu uliletwa na umoja. Maendeleo hayapatikani bila ya uhuru na umoja. Hivyo utamaduni kama nguzo ya umoja, ni chombo cha maendeleo (Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana, 1979, uk. vii)".

Kama jitihada za kukuza utamaduni, Mwalimu alianzisha Baraza la Kiswahili la Taifa (Bakita) mwaka 1967, hiyo ikiwa ni miaka sita tu baada ya uhuru, ili kukuza Kiswahili kiwe lugha inayoweza kutumiwa katika nyanja zote za jamii, utawala, elimu, mafunzo na biashara.

Miaka nane baadaye Serikali ya Mwalimu ilianzisha Baraza la Sanaa la Taifa na Baraza la Muziki la Taifa, ambayo yaliunganishwa mwaka 1984 kuwa Baraza la Sanaa la Taifa la sasa (Basata).

Madhumuni ya Basata na mabaraza yaliyolitangulia yalikuwa kufufua, kuendeleza na kukuza sanaa za asili (utamaduni) za Watanzania.

Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilianzisha masomo ya sanaa tangu mwaka 1966. Mwaka 1973, mafunzo ya sanaa kwa walimu wa shule za msingi yalianzishwa katika Chuo cha Ualimu Chang'ombe, Dar es Salaam na baadaye kuhamishiwa katika Chuo cha Ualimu Butimba Mwanza.

Chuo cha Sanaa Bagamoyo, sasa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni (TaSUBa), kilianzishwa mwaka 1981 kwa lengo la kutoa mafunzo kwa wasanii ili kuuenzi utamaduni. Aidha mwaka 1985 serikali ilianzisha matamasha na mashindano ya fani mbalimbali za utamaduni kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa, kanda hadi taifa.

Katika duru nyingi za kimataifa, nchi yetu chini ya Mwalimu ilisifiwa sana kwa jitihada zake za kushughulikia ukuzaji wa utamaduni.

Lakini sasa tumejikuta tukiangukia kule kule alikosema Mwalimu Nyerere kuwa 'kusanyiko la watu wasio na roho'. Tunapotea taratibu tukibaki kuwa taifa lisilo na utamaduni wake, lenye raia wasio na mwelekeo, wasiojifahamu, wasio na fahari ya utaifa wao, wasio na umoja, uzalendo, mshikamano au heshima mbele ya mataifa mengine. Pengine fani moja ya utamaduni ambayo bado inaonekana vyema ni Lugha ya Kiswahili.

Kwa kawaida utamaduni huipa jamii utambulisho. Sura na haiba ya jamii hueleweka na kuelezeka kutokana na utamaduni wa watu wake. Utamaduni hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kupitia lugha, sanaa na imani.

Mwalimu alihakikisha utamaduni wetu haupotei bali unaendelezwa na alijua kuwa nyenzo ya kuuendeleza ni kuanzisha Vituo maalumu vya Jumuiya vilivyojengwa katika kila wilaya maarufu na vilijulikana kama Community Centres.

Vituo vya jumuiya viliwekwa chini ya Maofisa Utamaduni kuvisimamia na kuwa mahala ambapo serikali ilipatenga maalumu kwa ajili ya shughuli za sanaa na kutafiti masuala yaliyohusu utamaduni: Lugha, Mila na Desturi katika ngazi ya Wilaya.

Vituo vya jumuiya au vituo vya kijamii yalikuwa maeneo ya umma ambapo wanajumuiya walikuwa wanakusanyika kwa shughuli za vikundi, usaidizi wa kijamii, habari za umma, na madhumuni mengine.


Leo hii vituo hivyo havipo tena baada ya kugeuzwa aidha kuwa ofisi za Manisipaa au kukodishwa kwa watu binafsi ili kuongeza pato la serikali za mitaa bila kujali vijana waliomo katika Manispaa wanapewa sehemu nyingine maalumu kufanya shughuli zao za sanaa.

Kukosekana kwa vituo hivyo vya kijamii na suala la Maofisa Utamaduni kuwa chini ya Tamisemi badala ya Idara mama ya Utamaduni ni mambo ambayo, tupende tusipende, yamechangia kuudidimiza utamaduni na sanaa nchini.

Utamaduni ukilelewa vizuri ni chombo chenye nafasi nyingi sana za ajira, huweza kuongeza pato la eneo husika kwa kuhamasisha maendeleo, huleta uzalendo, ubunifu wa mambo mbalimbali ya utamaduni, huweza kuhamasisha utalii katika utamaduni, na ni sehemu ya utalii ambayo kwa bahati mbaya sana haijatumika kikamilifu katika kuongeza kipato cha nchi hii kwa ujumla.

Nina matumaini makubwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ataendeleza pale alipoishia Mwalimu Nyerere kwani tangu ameingia madarakani Machi 19 mwaka 2021 nimeanza kuiona taswira ya Mwalimu Nyerere na utamaduni wetu.

Kama ambavyo amefanya kwenye Tamasha la Kizimkazi alililoliasisi miaka kadhaa iliyopita kule Kizimkazi Zanzibar ambako masuala ya utamaduni, mila na desturi zetu yanazingatiwa kwa kiwango cha juu.



# Msondo kuadhimisha miaka 60 ya kuzaliwa





**Na Hamid Yassin**

BENDI kongwe ya Msondo Ngoma Oktoba 26 itafanya onyesho kamambe kwenye Ukumbi wa Gwambina (zamani TTC) Chang'ombe katika sherehe yao ya kutimiza miaka 60 tangia kuanzishwa kwake .

Meneja wa bendi hiyo, Said Kiberiti amelipasha Uelekeo kuwa, siku hiyo kutakuwa na onyesho kali ambapo nyimbo zao zote tangu zile za mwaka 1964 ilipoanzishwa zitapigwa.

"Siku hii ni muhimu na adhimu kwetu sote Wana -Msondo Ngoma kwa ajili ya kutafakari na kukumbuka historia ya bendi yetu na taifa letu kiujumla, niwaombe wadau na wapenzi wa bendi yetu pendwa ni wakati wetu wa kuonyesha umoja wetu katika tukio hili," amesihi Kiberiti.

Kiberiti ambaye pia ndiye Katibu Mkuu wa Chama cha Muziki wa Dansi (CHAMUDATA), amevitaja viingilio vya tamasha hilo kama ifuatavyo; VVIP itakuwa Sh. 100,000, VIP itakuwa Sh. 50,000 na kawaida ni Sh. 15000.

Kiberiti amesema kuwa, kwa wale watakaokata tiketi siku ya tamasha kiingilio kutakuwa Sh. 20,000. Pia mpaka sasa vikundi mbalimbali vya burudani vimethibitisha kushiriki katika tamasha hilo na muda si mrefu vitatangaziwa rasmi.

Kiberiti amepasha kuwa, kwa wale wanaotaka kukata tiketi mapema wawasiliane na mhasibu wao wa bendi aitwae Anthony au kupitia Kundi la Whats Up la Msondo Ngoma wawasiliana na Mwekehazina wao Mwakidosho.

"Niwasihi washabiki na wadau wa bendi yetu pendwa, siku hiyo tuonyeshe mshikamano wetu ili watu wajue hii ni bendi kubwa," amesihi Kiberiti.

Pia Kiberiti amesema kuwa, Oktoba 13 kutakuwa na kisomo cha kuwarehemu wapendwa wao waliotangulia mbele za haki ambapo shughuli hiyo itafanyika ofisini kwao Amana Ilala kuanzia saa 4 asubuhi.

Msondo Ngoma wamepanga kuweka kambi mkoani Dodoma kwa wiki nzima na itaondoka Oktoba 18 na kurejea tarehe 24 mwezi huu na siku ya Alhamisi tarehe 25watafanya mkutano na waandishi wa habari pamoja na kukagua mitambo.

# Mama Diddy avunja ukimya

**NEW YORK, Marekani**

MAMA mzazi wa Diddy, Janice Combs, amevunja ukimya kwa mara ya kwanza kuhusu matatizo ya kisheria na mashtaka yanayomkabili mwanaye ambaye kwa sasa yuko gerezani hapa Brooklyn New York kwa mashtaka ya ulaghai, unyanyasaji wa kingono, na usafirishaji wa binadamu.

Janice alitoa taarifa yake kwa 'Local 10 News" siku ya juzi Jumapili kupitia Wakili Natlie Figgers. Aliongea maneno makali ya uchungu kuhusu jinsi jamii inavyomchukulia mwanaye na kumhukumu kabla ya kusikia upande wake wa pili na kusikilizwa kwa kesi yake.

"Ninakuja kwako leo kama mwingine ambaye nimehuzunishwa sana na tuhuma zinazotolewa dhidi ya mwanangu, Sean Combs. Inahuzunisha kuona mwanangu akihukumiwa si kwa ukweli, bali kwa simulizi iliyotengenezwa kutokana na uongo.

"Kutoa ushahidi kuonekana ana hatia hadharani kabla hajapata fursa ya kuthibitisha kutokuwa na hatia, ni maumivu ambayo hayawezi kuvumilika kwa maneno. Kama kila mwanadamu, mwanangu anastahili kuwa na siku yake atakayosimama mahakamani, hatimaye kushiriki upande wake, na kuthibitisha kutokuwa na hatia."

"Wakati mwingine, ukweli na uwongo hufungamana kwa karibu sana hivi kwamba inatisha kukubali sehemu moja ya hadithi, hasa wakati ukweli huo hauko kawaida au ni mgumu sana kuamini," Janice alisema.

Pia kwenye taarifa yake alisema mtoto wake huyo wa kiume mwenye umri wa miaka 54 anaweza kuwa alidanganya kuhusu unyanyasaji ambao ulinaswa kwenye video na CNN, lakini hiyo haimaanishi kuwa ana hatia ya unyanyasaji wa kijinsia anaotuhumiwa.

Kumbuka kwamba Jumanne iliyopita pia waathiriwa wengine 120 waliibuka na kudai kufanyiwa matukio ya unyanyasaji na rapa huyo katika nyakati tofauti tofauti.

Wakati huo huo, orodha ya wanaodaiwa kuwa washirika wa msanii wa Diddy Combs anayetuhumiwa kwa makosa ya unyanyasaji, ulaghai na biashara ya ngono, inatazamiwa kutajwa hivi karibuni katika hatua nyingine ya kesi zinazomkabili, Wakili mtetezi wa Waathirika wa matukio hayo Tony Buzbee amethibitisha.

Buzbee ameviambia vyombo vya habari kuwa; "majina hayo yatawashtua." Wakati akitangaza kesi mpya zilizofunguliwa dhidi ya Msanii huyo kwa niaba ya waathiriwa 120 wanaodai kunyanyaswa kingono na Diddy, amesema "siku itakuja ambapo tutataja majina mengine isipokuwa Sean Combs, na kuna majina mengi." amedokeza.

Wakili huyo ameongeza kuwa, kwa sasa ana mpango wa kuwasilisha kesi hizo katika majimbo kadhaa kwa muda wa siku 30 zijazo na ameahidi kufichua majina hayo baadaye pia amethibitisha kuwa nusu ya Walalamikaji ni Wanaume na kwamba mashambulizi mengi yanayodaiwa yalifanyika New York, California, Georgia na Florida.

Malalamiko 120 ambayo ametangaza kwa sasa yanaanzia katika kesi za mwaka 1991 huku mshukiwa mdogo kabisa anayedaiwa kunyanyaswa na msanii ametajwa kuwa ni mtoto wa umri wa miaka tisa tu, huku wanaomshtaki Diddy wengine 25 wakisema kuwa walikuwa watoto wadogo wakati msanii huyo anawatendea uhalifu huo.



Haya yote yanakuja baada ya Diddy mwenye umri wa miaka 54 kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Shirikisho hapa nchini Marekani kwa makosa ya ulaghai na biashara ya ngono.

Hata hivyo, msanii huyo amekanusha makosa yote na amekana hatia ya madai ya jinai huku akiendelea kushikiliwa katika gereza la Metropolitan bila dhamana.

# Mwalimu Nyerere alipenda michezo, akatibuliwa!

**Na Hamid Yassin**

KWA kuwa nimepata bahati ya kuona masuala ya michezo katika Awamu zote Sita za uongozi wa taifa letu, basi sio vibaya angalau kidogo sana nikakusimulia kuhusu michezo enzi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye tarehe 14 mwezi huu tutaadhimisha miaka 25 tangu atangulie mbele ya haki.

Ni wazi Serikali ina uwezo mkubwa wa kuua, kudumaza, kuuhuisha au kuendeleza michezo katika nchi yoyote ile duniani, sisi Tanzania tuna bahati ya mtende kupata viongozi waliopenda wanaopenda michezo.

Katika Utawala wa awamu ya kwanza chini ya Rais wa kwanza Mwalimu Nyerere, michezo ilipewa kipaumbele ilichostahili katika nyanja zote.

Kamwe huwezi kuendeleza michezo bila miundombinu yake, hakuna shaka kwamba, ni wakati awamu hii ya kwanza ndipo viwanja vingi vya michezo tuvionavyo leo kote nchini vilijengwa tena kwa nguvu za wananchi.

Uhuru, Karume Dar es salaam (sasa wa TFF), Kirumba Mwanza, Jamhuri Dodoma, Kambarage Shinyanga, Shekh Amri Abeid Arusha, Lake Tanganyika Kigoma, Ushirika Moshi, Mkwakwani Tanga, Majimaji Songea, Sokoine Mbeya ni baadhi tu ya viwanja vilivyojengwa wakati wa awamu yake ya kwanza.

Ukichukua viwanja alivyoviacha na vilivyojengwa baadaye ni wazi utakubaliana na mimi huyu Mwalimu Nyerere alikuwa na nia ya dhati ya michezo na aliitekeleza kwa vitendo.

Ni katika kipindi chake kila shirika aidha liwe la umma au binafsi ilikuwa ni lazima liwe na timu za michezo.

Hapa ndipo tulipopata timu kama Plisner, Sigara, Reli, Tumbaku, RTC Kagera, RTC Kigoma, Biashara Mwanza, Biashara Shinyanga, Pamba, Tanarees, TPC Moshi, Ushirika Kilimanjaro, Ufi, BP, Maziwa, Urafiki, Fishnert, Ngozi, Bora, Kago, Bandari Dar, Bandari Mtwara na nyingine nyingi kote nchini.

Wachezaji wengi waliibukia timu hizi na kuja kuwa wachezaji wakubwa waliokuja kulitumikia Taifa.


Nakumbuka baada ya vita vya Uganda, Serikali ya Uganda ilituma wajumbe kuja kujifunza kwetu sera za michezo na jinsi ya kuzitekeleza. Kile Uganda walichokuja kujifunza kwetu ndicho wanakisimamia mpaka leo.

Hayati Mwalimu Nyerere alihakikisha viwanja vya michezo vyote vinavyokidhi vigezo vinakuwepo vingi vya kutosha kila mkoa hapa nchini. Shule zote za msingi na sekondari ilikuwa ni lazima ziwe na viwanja.

Mitaani kote viwanja vilikuwepo, mashirika yote ya umma na binafsi ilikuwa ni lazima kila shirika liwe na uwanja. Ndio maana leo vimebaki baadhi kama Kinesi ( Urafiki), TTC Chang'ombe, Bandari kule Temeke, nk.

Viko wapi viwanja vya Ufi, Fishnert, Maziwa, Chibuku nk? Bado vipo? Na bado vinakidhi vigezo vya kuitwa viwanja vya michezo? Hapana havipo. Nini kilitokea? Wajuaji walibadilisha matumizi ya viwanja hivyo!

Enzi za Mwalimu alihakikisha michezo inachezwa, na inakuwa ni michezo yenye ushindani wa kutosha kuanzia, mashuleni, timu za vijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa mpaka taifa..



**Hayati Mwalimu Julius Nyerere akicheza bao na jirani yake Msasani huku Rais wa awamu ya pili, hayati Ali Hassan Mwinyi, mkewe Mama Maria Nyerere wakishuhudia.**

Ziko wapi timu za mikoa zilizotuibulia wachezaji kutoka mikoa yao? Ziko wapi timu za mikoa kama Mzizima United, Ingebensabo, Mashujaa wa Unyanyembe, Kindai Shooting Stars, Mont Meru Warious, Kilimanjaro Stars, nk? Kwa nini mashindano yale ya taifa ya mikoa yalikufa? Ni kweli michuano ya Kombe la Taifa ilikuwa haina tija yoyote kwenye soka letu?

Kwa nini Mwalimu Nyerere alifanikiwa kuvianzisha viwanja na kuvilinda? Kwa nini siku hizi vimevamiwa na kujengwa vitu vingine? Nani wa kulaumiwa?

Hakuna wa kulaumiwa bali ni sisi wenyewe wa kushindwa kuwa na maono ya Baba wa Taifa na kuzijali tamaa zetu zaidi na ubinafsi. Tulifika mahali tukaamini kuweka biashara, darasa, au baa kwenye eneo la uwanja wa michezo tukidhani ndio maendeleo.

Na kibaya zaidi tukashirikiana na mamlaka kuhujumu viwanja kwa njia chafu na ovu. Ninaamini huko alipo kama Baba wa Taifa anaona basi atakuwa analia machozi yasiyokoma.

Tumeshindwa kuenzi mazuri ya michezo ya Baba wa Taifa na tumeamua kuharibu kila kitu kwa tamaa zetu. Viwanja vya michezo vimegeuzwa vya biashara ya kupaki magari karibu kote nchini. Inauma na kusikitisha sana.

Kama tunataka kufanikiwa kwenye michezo kama nchi lazima turudi pale tulipopotea njia tukaitafute njia yetu.

Turudi kuhakikisha kila shule ya msingi ina uwanja, ina mipira, ina waalimu wa michezo waliosomea ambao wao wenyewe wanaipenda michezo.

Na kuwe na michezo ya kutosha mashuleni yenye ushindani wa shule na shule, kata kwa kata, wilaya kwa wilaya mpaka mkoa kwa mkoa. Kama hatuwezi kurudi hapa basi tukubali njia tumeipoteza na hatuijui tena. Hivyo tukubali kuzidi kupotea tukiingia maporini zaidi.

Hayati Mwalimu alikuwa anapenda sana michezo na wakati wa uongozi wake ndipo wanamichezo wa Tanzania walipotamba ndani na nje ya mipaka yetu.

Rekodi zote za kwenye michezo yote ikiwemo riadha, ngumi na soka ziliwekwa wakati wa Awamu ya Kwanza. Wakina Fielbert Bayi, Gidamasi Shahanga, Selemani Nyambui na mabondia marehemu Titus Simba, Willy Isangula, Michael Isangula waliweka rekodi kubwa kwenye michezo ya Olimpiki na Jumuiya ya Madola enzi zile za Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere.

Taifa Stars iliingia fainali za Kombe la Mataifa Huru ya Afrika (sasa Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON) kwa mara ya kwanza enzi ya Mwalimu Nyerere mwaka 1980 na baada ya hapo tulikaa bila kufuzu kwa zaidi ya miaka 35!

### TULIMUUDHI AKIWA HAI

Kama nilivyosema hapo juu kuwa, Mwalimu alipenda sana michezo na alikuwa anahudhuria viwanjani, lakini mwaka 1979 viongozi wa wakati huo wa soka walimchefua pale alipokuwa mgeni wa heshima kwenye pambano la timu ya taifa, Taifa Stars, dhidi ya timu ya taifa ya Sudan na wachezaji wa Stars kucheza kifua wazi!

Mwalimu akiwa na mgeni wake pale Uwanja wa Uhuru Rais wa Sudan wa wakati huo hayati, Jaafar Nimeiry, Stars iliingia uwanja kidari wazi kwa mshangao wa Mwalimu Nyerere mbele ya mgeni wake, Nimeiry.


Viongozi wa FAT wakati huo wakiongozwa na Mwenyekiti wao marehemu, Said El Mamry walidai jezi za Stars na Sudan zilifanana ndipo wakaamua mwenyeji acheze kifua wazi! Jezi zilithe letwa wakati wa mapumziko lakini Mwalimu Nyerere hakusubiri kuangalia hicho kipindi cha pili, kwa hasira akamchukua mgeni wake Rais Nimeiry wakaondoka uwanjani.

Tangu wakati huo Mwalimu Nyerere hakuhudhuria tena mchezo wowote wa soka au mwingineo, akaamua kubaki kushabikia na kucheza mchezo wa bao ambapo alikuwa nguli wa mchezo huo wa bao na mingine ya jadi.



**Aliyekuwa Rais wa Sudan, Hayati Jaafar Nimeiry akikagua timu ya Taifa huku wachezaji wakiwa kifua wazi. Hapa ndipo Mwalimu Nyerere alipokasirika na kususa kwenda viwanjani.**

## Kona ya Urembo



# Urembo wa nywele kwa mwanaume mtanashati

**Na Hidaya Machupa**

KWA mwanaume mtanashati, nywele ni sehemu muhimu ya mwonekano wa jumla, na zinachangia sana katika kufafanua mtindo wake wa maisha, hadhi yake, na jinsi anavyojitunza.

Urembo wa nywele unahusu si tu muundo wa nywele, bali pia usafi, afya, na uwezo wa kuzitunza kwa njia inayodumisha uhalisia na ustaarabu. Hapa chini ni makala inayozungumzia mbinu bora za urembo wa nywele kwa mwanaume mtanashati.

Mwanaume mtanashati anatakiwa kuchagua mtindo wa nywele unaoendana na sura ya uso wake, hali ya maisha yake, na hata fani anayojishughulisha nayo. Kuna mitindo mbalimbali inayoweza kuonyesha mtindo wa maisha ya kifahari, mfano:-

### MTINDO WA UNDERCUT AU FADE

Ni maarufu kwa sababu unaonyesha mwonekano nadhifu na wa kisasa. Nywele hukatwa kwa ufupi pembeni huku juu zikibakia ndefu kidogo kwa mpangilio mzuri.


### SLICK BACK

Ni mtindo wa kurudisha nywele nyuma kwa kutumia mafuta ya 'gel' au 'pomade' ili kuzipanga vizuri. Huu ni mtindo unaotoa picha ya ujasiri na uthabiti.

### POMPADOUR

Huu ni mtindo wa kurudisha nywele juu na nyuma, huku zikiwa na ujazo wa kutosha. Inafaa kwa wanaume wenye nywele nene na wenye sura ndefu.

Mtindo wowote utakaouchagua, hakikisha unaendana na kazi yako na maisha yako ya kila siku. Mwanaume anayejali urembo wa nywele zake anatakiwa kuzingatia uwiano wa usafi na mtindo.



### KUOSHA NYWELE MARA 2-3 KWA WIKI

Hii itasaidia kuondoa uchafu, na jasho kutoka kwenye nywele na ngozi ya kichwa. Hakikisha unatumia shampoo na 'conditioner' zenye viambato vya asili ili kudumisha afya ya nywele zako.

### MAFUTA YA NAZI

Mafuta haya husaidia kulainisha nywele, kuzipa unyevu na kuzuia ukavu unaoweza kusababisha nywele kuwa na mwonekano mbaya au kugawanyika.

Ili kudumisha mwonekano safi, mwanaume mtanashati anapaswa kutembelea kinyozi wake angalau mara moja kila wiki mbili hadi tatu. Hii inasaidia kudhibiti mweleko wa nywele na kuzuia kuziharibu.

Pia, ni muhimu kuzingatia usafi wa mashine au vifaa vinavyotumika kukata nywele ili kuepuka maambukizi ya ngozi.

Urembo wa nywele sio tu za kichwani, bali pia sehemu ya ndevu na sharubu. Hizi zinahitaji matunzo bora.

Kuweka ndevu na sharubu katika umbo linaloendana na mwonekano wako wa sura ni muhimu. Wanaume walio na ndevu wanahitaji kuzichana kila siku na kutumia mafuta ya ndevu (beard oil) ili kulainisha nywele na kuimarisha afya ya ngozi chini ya ndevu.

### KUOSHA NA KUZILAINISHA

Osha ndevu zako mara kwa mara kwa shampoo maalum ya ndevu, na utumie mafuta ya ndevu kuhakikisha zina unyevu wa kutosha ili zionekane laini na zenye mvuto.

Afya ya nywele hutegemea sana lishe. Mwanaume mtanashati anaweza kupata nywele zenye afya na kung'aa kwa kufuata mlo wenye virutubisho kama vifuatavyo.

### PROTINI

Inayopatikana kwenye nyama, samaki, mayai, na maharage. Protini husaidia katika ukuaji wa nywele na kuzifanya ziwe nene.

OMEGA-3

Asidi ya mafuta inayopatikana kwenye samaki wa maji baridi kama salmon, ambayo inachangia nywele zenye afya.

### VITAMINI A, C, NA E

Hizi vitamini ni muhimu kwa ukuaji wa nywele zenye nguvu na ngozi yenye afya.

Ikiwa mwanaume mtanashati anakumbwa na matatizo ya nywele kama kupoteza nywele au ukavu, ni muhimu kutafuta ushauri wa kitaalamu. Daktari wa ngozi au mtaalamu wa nywele anaweza kupendekeza bidhaa bora za nywele au matibabu maalum kama (minoxidil) kwa ajili ya kuongeza ukuaji wa nywele.

Mwanaume mtanashati anajua kuwa urembo wa nywele ni sehemu ya kujiamini. Nywele zinapokuwa safi, nadhifu, na zenye muundo mzuri, huongeza hisia za kibinafsi na kuvutia macho ya watu. Mwanaume anayejali nywele zake, kwa hakika anajali mwonekano wake wa jumla, jambo linaloongeza nafasi ya kufanikiwa kijamii na kitaalamu.

Mwanaume anapaswa kuwa msafi wa nywele kwa sababu mbalimbali zinazohusiana na afya, urembo, na heshima ya kijamii. Hizi ni sababu kuu zinazomfanya mwanaume awe makini na usafi wa nywele zake:



### KUIMARISHA MWONEKANO NA UREMBO

Nywele safi na zinazotunzwa vizuri zinaongeza mwonekano mzuri wa jumla wa mwanaume. Zinaweza kumpa mtu kujiamini na kuvutia machoni pa wengine.

Nywele zikiwa zimepangiliwa na zina afya, zinaonesha nidhamu ya mtu katika kujitunza, jambo ambalo linaathiri pia jinsi anavyokubalika kijamii na kibiashara.

### KUIMARISHA HESHIMA YA KIBINAFSI NA KIJAMII

Usafi wa nywele unaakisi kiwango cha nidhamu na heshima binafsi. Watu wengi hujihusisha zaidi na mtu ambaye anaonekana nadhifu na safi, na nywele safi ni sehemu muhimu ya picha hii ya nje.

Usafi huu unahusisha pia sehemu za ndevu na sharubu, ambazo zinaweza kutoa taswira ya mwanaume aliye makini na mwenye mpangilio.

Kwa mwanaume mtanashati, urembo wa nywele ni zaidi ya mtindo wa muda mfupi. Ni sehemu ya kujitunza, kujithamini, na kutoa picha bora kwa jamii inayomzunguka.

Kwa kufuata mbinu bora za utunzaji wa nywele na ndevu, pamoja na kuepuka bidhaa zenye kemikali kali, mwanaume anaweza kudumisha mwonekano safi, wa kisasa, na kuvutia.

Kwa kifupi, mwanaume kuwa msafi wa nywele sio tu suala la urembo, bali pia ni jambo la kiafya na kijamii. Huku kukiwa na manufaa ya kiafya, pia husaidia kujenga picha nzuri ya mtu katika jamii na kuimarisha heshima ya kibinafsi.





*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo Spoti

| Jumatano Oktoba 9-15, 2024 |

## Penzi la Harmonize, Poshi Queen layeyuka

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwepo kwa stori kuwa mahusiano ya wapendanao, Harmonize na Poshi Queen yamevunjika kutokana na wawili hao kupunguzana kwa mara ya pili kwenye mitandao ya kijamii, hatimaye mlimbwende Poshi amekiri kutokea kwa suala hilo.



Mrembo Poshi akifanyiwa mahojiano katika kipindi cha Amplifier cha Milllad Ayo amefunguka kuwa, ameachana na Harmonize ingawa amedai hawajagombana.

"Hamna sababu ni muda tu umeisha, hata sijui, ni hadithi ndefu, tulikubaliana tupeane muda wa kutokuwa pamoja, lakini wala hatujagombana," amekaririwa Poshi Queen katika mahojiano hayo.

# Simba: Mkapa utaendelea kuwa machinjio ya wageni

- **Ahmed: Tunawaheshimu wapinzani ila hawatatoka salama 'Lupaso'**
- **Yapambana Mpanzu acheze dhidi ya Bravo ya Angola Novemba 27**

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba imejitapa kuwa, wataendeleza ule moto wao wa kuziangamiza timu pinzani katika michuano ijayo ya Kombe la Shirikisho kwenye Uwanja wa nyumbani wa Mkapa.

Afisa Habari wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally ametamba kuwa, ingawa timu zote walizopangwa nazo pamoja kundi A hawajawahi kukutana nazo kwenye michuano yoyote ile, lakini wamepanga kuchukua alama zote tisa watakapocheza nyumbani Uwanja huo wa Mkapa.

"Kila atakayekuja Benjamin Mkapa ataacha alama tatu ataondoka, ila ugenini kati ya hawa watatu kuna wawili watatupa alama tatu tatu huko huko kwao, kwa maana alama sita halafu kuna mmoja anaweza akatuachia alama moja," amejinasibu Ahmed Ally.

Ahmed anapasha kuwa, wanaziheshimu timu zote tatu walizopangwa nazo, lakini ili Simba ifuzu bila tashititi wanatambua lazima kwanza wafanye vizuri kwenye uwanja wa nyumbani halafu kwenda kutafuta alama nyingine angalau tatu ugenini hapo watatinga robo fainali kwa kuongoza kundi lao.

"Hizi mechi za hatua ya makundi huwa zinachezwa kwa mahesabu makali, kwanza lazima uwe na uhakika wa kushinda mechi zako zote za nyumbani, kinyume na hapo mambo ya kuhesabu vidole kwa kutegemea matokeo ya mechi za timu nyingine yatatuhusu, jambo ambalo hatutaki litukute safari hii," ametanabahisha Ahmed.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya klabu hiyo, Mohamed MO Dewji amesema kuwa, wataendelea kupambana hadi watimize ndoto yao ya kutwaa ubingwa wa Afrika na kwa kuanzia wamepanga kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano haya wanayoshiriki ya Kombe la CAF kwa kufika mbali zaidi.

"Kila maono yana njia yake ingawa safari ni ndefu, maono hayafi. Yanaishi ndani ya mioyo yetu hadi yatimie. Kwa pamoja, tunaunda Simba yenye uwezo wa kushindana kimataifa na kuleta fahari kwa wanaSimba wote," ameandika MO Dewji kwenye Ukurasa wake wa Instagramu jana.

Amewataka Wanasimba kuwa pamoja katika kujenga Simba ya sasa na ya kesho.

Wakati huo huo, Simba inapambana kuhakikisha mchezaji wake mpya, Elie Mpanzu anacheza mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi hapo Novemba 27 dhidi ya timu ya Bravo ya Angola.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya Simba zinapasha kuwa, wanasubiri dirisha la usajili la CAF linalotarajiwa kufunguliwa hivi karibuni ili kuingiza jina la Mpanzu na kumkata kipa, Ayubu Lakred anayeandamwa na majeraha.

Imeelezwa kuwa, Mpanzu ataingia kwenye usajili rasmi na atacheza kimataifa pekee hadi pale dirisha dogo la usajili wa ndani litakapofunguliwa mwezi Desemba ndipo atacheza na Ligi Kuu ya NBC.

Simba imepangwa kundi A la michuano hiyo ya Makundi ya Kombe la CAF pamoja na timu za SC Sfaxien ya Tunisia, CS Constantine ya Algeria na FC Bravos de Marquis ya Angola.





## Mwenda bado akitamani kiti cha FKF

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Shirikisho la Soka la Kenya (FKF), Nick Mwendwa bado anashikilia msimamo wake kwamba atatetea kiti chake licha ya Wizara ya Michezo ya hapa Kenya kusema haiwezekani.

Mwendwa amesalia na msimamo mkali katika kuwania muhula wa tatu katika uchaguzi ujao wa kitaifa wa FKF uliopangwa kufanyika Desemba 7, 2024.

Bosi huyo wa FKF tayari amemaliza mihula miwili kulingana na sheria ya michezo ya mwaka 2013, lakini anasisitiza kuwa anastahili kuhudumu kwa muhula wa tatu.

Tangazo la Mwendwa linakuja kutokana na msimamo wa Waziri wa Michezo, Kipchumba Murkomen kwamba hakuna mtu ambaye tayari amehudumu kwa muhula wake wa pili ataruhusiwa kugombea wadhifa huo.

Waziri huyo alifika mbele ya Bunge la kitaifa mnamo Septemba 25 ambapo alithibitisha kwamba maafisa hao waliruhusiwa kugombea nyadhifa nyingine lakini si hizi wanazozishikilia hivi sasa.

# Yanga itatinga robo fainali kwa ubora wake




- **Chama atarajia mataji makubwa Afrika na 'Wananchi'**

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Yanga, Ally Kamwe amenena kuwa, kundi lao kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika si jepesi, lakini haitawazuia kutinga hatua ya robo fainali kutokana na ubora wa timu yao kwa sasa.

Kamwe amebainisha kuwa, Yanga imekuwa katika ubora wa hali ya juu katika misimu hii mitatu, hivyo hiyo ndiyo itakuwa silaha yao kubwa kuelekea kufuzu robo fainali ya michuano hiyo ya juu ngazi ya klabu barani Afrika.

"Hakuna timu ngeni hapo, karibu zote tumeshacheza nazo huko miaka ya nyumba, hawa TP Mazembe tuliwafunga mwaka juzi nje ndani, Al Hilal walituondoa kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika mwaka juzi na tukaangukia Shirikisho, hivyo huu ndiyo wakati wa kulipa kisasi kwa kikosi chetu hiki cha maangamizi cha sasa," ametamba Kamwe.

Akiwazungumzia wapinzani wao wengine kwenye kundi hilo A, MC Alger ya Algeria, Kamwe amepasha kuwa, hata hao wana kisasi nao baada ya kuwafunga bao 4-0 mwaka 2017 kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho na kuwatupa nje ya mashindano.

Wakati huo huo, kiungo mshambuliaji mpya wa Yanga, Clatous Chama ameelezea furaha yake ya kujiunga na klabu hiyo na kuisfia kwamba ni miongoni mwa klabu kubwa barani Afrika na anatarajia kutwaa mataji makubwa ya Afrika akiwa na kikosi hicho cha Wananchi.

"Siku zote napenda kufanya kazi na timu ya aina hii (Yanga). Hapa nina furaha na natarajia kushinda mataji makubwa. Kushinda kikombe cha CAF ni moja ya jambo lililonileta hapa Yanga na hilo linawezekana," amenena Chama katika mahojiano yake maalumu na Mtandao wa klabu hiyo.